JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

# Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura

Novemba 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

# Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura

**Novemba 2023**

| Imeidhinishwa Na; | Cheo | Sahii | Tarehe |
| --- | --- | --- | --- |
| DR. JABIRI K. BAKARI | MKURUGENZI MKUU | [signature] | 15-11-2023 |

# YALIYOMO


Ukurasa

VIELELEZO VILIVYOMO ..... vii

VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ..... viii

DIBAJI ..... x

1. UTANGULIZI ..... 1

1.1 Madhumuni ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura ..... 2

1.2 Mawanda ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura ..... 3

1.3 Malengo ya Muda Mrefu ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura ..... 3

1.4 Malengo ya Muda Mfupi ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura ..... 4

1.4.1 Kuandaa na kurasimisha muundo wa kufanya maamuzi ukiwa na majukumu yaliyobainishwa wazi kwa ajili ya kuratibu uwezo wa Mawasiliano ya dharura wakati wa maafa ..... 4

1.4.2 Kuimarisha uwezo wa mifumo ya Mawasiliano (Redio, TV, na Mashirika ya Simu za Mkononi kwa kuunganisha na kuboresha mwitikio wa Watoa Huduma za dharura/maafa ..... 5

1.4.3 Kuhakikisha kuwa watoa huduma za dharura wanaweza kuwasiliana katika tukio ambalo Mawasiliano ya kawaida yana changamoto ..... 6

1.4.4 Kutoa mafunzo ya kutosha, endelevu na vipindi vya mafunzo ya dharura kwa vitendo ..... 7

1.4.5 Ushirikiano wa Kimataifa ..... 7

2. NAFASI YA MAWASILIANO KATIKA KUDHIBITI MAAFA ..... 9

2.1 Matumizi ya Mawasiliano katika Kupunguza Maafa ..... 9

2.1.1 Muhtasari wa Maafa nchini Tanzania ..... 10

2.1.2 Uchambuzi wa Vihatarishi vya Miundombinu ya Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA ..... 12

2.1.3 Kupunguza Athari na Kuimarisha Uthabiti wa Mitandao ya Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA ..... 12

2.1.4 Mfumo wa Kisheria na Udhibiti ..... 12

A. Utoaji Leseni za Huduma ya Mawasiliano /TEHEMA ..... 12

B. Uwekaji wa Mpangilio wa Mawimbi ya Redio, Usambazaji na Uidhinishaji ..... 13

C. Matumizi ya Pamoja ya Miundombinu ..... 13

2.2 TEHAMA/Mawasiliano ya Simu katika Awamu ya Maandalizi ya Maafa ..... 13

2.2.1 Mfumo wa TEHAMA wa Kukabiliana na Maafa ....................14
2.2.2 Kuwa na Mfumo wa Simu Hawilishi za Kipaumbele....................16
2.2.3 Vifaa na Namba za Dharura ....................17
2.2.4 Vitahadharishi Awali na Mifumo Inayohamasisha....................17
2.2.5 Utumaji wa Arafa kwa ajili ya Tahadhari kwa Umma ....................18
2.2.6 Protokali Jumuishi ya Kutahadharisha (CAP) ....................19
2.2.7 Uwezo wa Kufanya Maandalizi ya Kukabiliana na Maafa....................20
2.2.8 Mipango ya Kukabiliana na Dharura....................21
2.2.9 Mitandao ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi/TEHAMA kwa ajili ya Ufuatiliaji wa Mifumo ya Tahadhari na Vitahadharishi vya mwanzo....................22
2.2.10 Mawasiliano ya Simu za Mkononi/TEHAMA katika Udhibiti wa Maafa na Upunguzaji wa Vihatarishi....................22
2.2.11 Matumizi ya Mawasiliano/ ya SimuTEHAMA na Tasnia ya Utangazaji katika Kuongeza Uelewa ....................23
2.2.12 Ushirikiano na Wadau Mbalimbali (Sekta za Umma na Binafsi)....................23
2.2.13 Mafunzo kwa Vitendo....................24
2.2.14 Msaada kwa Watu Wenye Mahitaji Maalum ....................25
2.2.15 Taratibu Bora za Utendajikazi (SOP)....................25
2.2.16 Orodha ya Maofisa wa Mawasiliano ....................26
2.3 Awamu ya Kukabiliana na Dharura na Maafa ....................26
2.3.1 Tamko la Dharura....................26
2.3.2 Ukusanyaji na Uchambuzi wa data/taarifa kuhusiana na mahitaji ya haraka........33
2.3.3 Uelewa wa Kimazingira na Uhuishaji wa Taarifa ....................33
2.3.4 Kuunganisha familia na marafiki....................33
2.3.5 Ukusanyaji Pamoja wa Vifaa ....................34
2.4 Afua Zinazotolewa Wakati wa Udhibiti wa Dharura na Maafa ....................34
2.4.1 Tathmini ya Taarifa za Uharibifu na Mahitaji....................34
2.4.2 Kujenga Upya na Kuboresha Miundombinu ya Mawasiliano/TEHAMA ....................35
2.4.3 Kuunganisha Njia Mbadala na za Ziada katika Mitandao ya Mawasiliano/TEHAMA ....................35
2.4.4 Kutambua maeneo yanayohitaji msaada wa urejeshaji na shughuli za ufuatiliaji wa afua ....................36
2.4.5 Kuratibu Shughuli za Ujenzi Upya ....................36

3. MPANGO WA UTEKELEZAJI NA VIPIMO ....................................................... 36
3.1 Taarifa za Majanga Mbalimbali ....................................................... 36
3.2 Taarifa za Matumizi ya Teknolojia Mbalimbali ....................................................... 37
3.3 Taarifa za Ushirikiano wa Wadau Mbalimbali ....................................................... 37
3.4 Taarifa za Utekelezaji wa Awamu Mbalimbali ....................................................... 37
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC) 41
3.5 Mapitio ya Mpango ....................................................... 43
4. HITIMISHO ....................................................... 43
KIAMBATISHO I: SOP KWA AJILI YA MAWASILIANO YA DHARURA ....................................................... 44
1.0 UTANGULIZI ....................................................... 44
1.1 Malengo ....................................................... 44
1.2 Vyombo/Asasi Muhimu ....................................................... 44
2.0 MCHAKATO WA UTOAJI TAHADHARI KWA UMMA ....................................................... 45
2.1 Utumaji wa Arafa ....................................................... 45
2.2 Matangazo ya Redio na Televisheni ....................................................... 45
2.3 Tovuti ya Idara ya Menejimenti ya Maafa (DMD) ....................................................... 45
2.4 Chaneli za Mitandao ya Kijamii (Facebook, Twitter, Instagram, Youtube na Blogu) 45
Facebook ....................................................... 46
Twitter ....................................................... 46
Akaunti ya Instagram ....................................................... 46
Akaunti ya YouTube ....................................................... 46
Blogu ....................................................... 46
3.0 MAWASILIANO YA REDIO (Masafa Marefu, Masafa Mafupi na ya Kati) ....................................................... 46
3.1 Redio ya Masafa Marefu na za Masafa Mafupi na ya Kati ....................................................... 46
3.2 Ratiba ya Majaribio: ....................................................... 48
4.0 MAWASILIANO YA SATELAITI ....................................................... 48
4.1 Simu za Satelaiti ....................................................... 48
4.2 Kituo Kidogo Sana Kinachopitisha Mawimbi ya Data, Sauti na Video za Satelaiti (VSAT) ....................................................... 48
5.0 MFUMO WA USAFIRI WA ANGA USIOKUWA NA RUBANI (DRONES) ....................................................... 49

KIAMBATISHO II: MAOFISA WENYE WAJIBU WA KUTOA HUDUMA ZA MAWASILIANO KATIKA VITUO VYA KUDHIBITI MAAFA....................................49

B. Taarifa za Mawasiliano ya Viongozi/Watu wa Kuwasiliana nao Kitaifa (Mkoa, Wilaya)........................................................................................................49

C. Taarifa za Mawasiliano ya Watoa Huduma za Mawasiliano wanaohusika na dharura na maafa........................................................................................................49

KIAMBATISHO III: TAARIFA KUHUSIANA NA KUTOKEA KWA MAAFA.....................50

## VIELELEZO VILIVYOMO

Kielelezo cha 1: Awamu za Kudhibiti Maafa ........ 9

Kielelezo cha 2: Utokeaji wa majanga ya asili kwa aina zake nchini Tanzania katika miongo miwili iliyopita kuanzia 1997 hadi 2017 ........ 11

Kielelezo cha 3: Idadi ya watu walioathiriwa na mafuriko kwa mujibu wa hali ya tabia ya nchi iliyopo na inayokuja ........ 11

Kielelezo cha 4: Mfumo wa Taarifa za Kukabili Maafa ........ 16

Kielelezo cha 5: Protokali ya Kutahadharisha Kawaida ........ 20

Kielelezo cha 6: Taratibu za utoaji wa huduma za Mawasiliano ya simu za dharura...... 27

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| CAP | Protokali Jumuishi ya Kutahadharisha (*Common Alerting Protocol*) |
| CRASA | Chama cha Wasimamizi wa Mawasiliano Kusini mwa Afrika (*Communications Regulators' Association of Southern Africa*) |
| DMD | Idara ya Menejimenti ya Maafa – DMD (*Department of Disaster Management*) |
| EGA | Mamlaka ya Serikali Mtandao (*Electronic Government Authority*) |
| EOCC | Kituo cha Mawasiliano na Utendajikazi wa Dharura (*Emergency Operational and Communication Centre*) |
| EWS | Mfumo wa Tahadhari za Kabla (*Early Warning System*) |
| GST | Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*Geological Survey of Tanzania*) |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano - *TEHAMA* (*Information and Communication Technology*) |
| IOC | Kituo cha Utendajikazi wa Kiintelijensia (*Intelligent Operations Centre*) |
| ISP | Watoa Huduma za Intaneti (*Internet Service Operators*) |
| ITU | Shirika la Umoja wa Mawasiliano ya Kimataifa (*International Telecommunication Union*) |
| ITU-T | Sekta ya Viwango vya Mawasiliano ya Shirika la Umoja wa Mawasiliano ya Kimataifa (*International Telecommunication Union -Telecommunication Standardization Sector*) |
| MICIT | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (*Ministry of Information, Communication and Information Technology*) |
| MNOs | Watendajikazi/Waendeshaji wa Mitandao ya Simu za Mkononi (Mobile Network Operators) |
| MDAs | Wizara, Idara na Mashirika (*Ministries, Departments and Agencies*) |
| NETP | Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura (*National Emergency Telecommunication Plan*) |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*National Environmental Management Council*) |
| NGOs | Asasi Zisizokuwa za Serikali – AZISE (*Non-Governmental Organisations*) |
| PMO | Ofisi ya Waziri Mkuu – OWM (*Prime Minister's Office*) |
| PPDR | Sekta ya Ulinzi wa Watu/Umma na Misaada ya Maafa (*Public Protection and Disaster Relief*) |
| PORALG | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa OR - TAMISEMI (*President's Office Regional Administration and Local Government*) |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Southern African Development Community*) |

| | |
|---|---|
| SOPs | Taratibu Bora za Utendajikazi (*Standard Operating Procedures*) |
| TCAA | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*Tanzania Civil Aviation Authority*) |
| TAA | Tanzania Airport Authority |
| TASAC | Tanzania Shipping Agencies Corporation |
| TCRA | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*Tanzania Communications Regulatory Authority*) |
| TMA | Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania (*Tanzania Meteorological Authority*) |
| TPDF | Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania – JWTZ (*Tanzania People's Defence Force*) |
| TRCS | Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (*Tanzania Red Cross Society*) |
| UAV | Ndege Zisizokuwa na Rubani (*Unmanned Aerial Vehicles*) |
| UN | Umoja wa Mataifa (*United Nations*) |
| VSAT | Kituo Kidogo Sana Kinachopitisha Mawimbi ya Data, Sauti na Video za Satelaiti) (*Very Small Aperture Terminal*) |

## DIBAJI

Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura (NETP) ni mpango wa kimkakati ulioandaliwa ili kudhibiti vyema vihatarishi vya maafa wakati wa hatua za kuvipunguza, kufanya maandalizi, kukabiliana navyo na katika awamu za urejeji wa hali kwa kuimarisha Mawasiliano na upashanaji habari kote Serikalini, ndani ya jamii iliyoko kwenye vihatarishi hivyo na kati ya umma/jamii na mashirika binafsi.

Ili kuzuia au kupunguza vifo au uharibifu wa mali na/au maliasili kabla, wakati na baada ya maafa au dharura, Idara ya Menejimenti ya Maafa iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ilianzisha Kituo cha Mawasiliano na Utendajikazi wa Dharura (EOCC) chenye Taratibu zake Bora za Utendajikazi (SOPs) ili kuongoza na kusimamia utendajikazi wa saa 24/7. Hii ni katika kutambua kuwa maafa yanapotokea, uratibu na Mawasiliano madhubuti ni masuala ya muhimu katika kukabiliana na maafa kwa haraka na kwa wakati.

Kila mdau wa Maafa au Dharura amepewa majukumu, wajibu na kazi kama inavyofafanuliwa katika SOP ambapo jukumu la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) limejikita kwenye utoaji wa huduma za Mawasiliano na Tahadhari kwa umma. TCRA inashirikiana na wadau wengine katika kupanga na kuandaa NETP ambayo itaisaidia Idara ya Menejimenti ya Maafa (DMD) iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kuwezesha uratibu mzuri wa shughuli wakati wa hatua za kuyapunguza, kufanya maandalizi, kukabiliana nayo na katika awamu za urejeji wa hali.

Mpango huu umeandaliwa ili:

i Kutambua uwezo unaohitajika kwa watoa huduma za dharura ili kuhakikisha kuna utangamano na upatikanaji wa huduma za Mawasiliano kabla, wakati na baada ya dharura na kutambua vikwazo katika usambazaji na matumizi ya mifumo ya Mawasiliano;

ii Kupendekeza usanidi wa mifumo muhimu ya Mawasiliano tangamano inayohitajika kwa watoa huduma za dharura ili kukabiliana nazo kwa ufanisi pamoja na matukio mengine mbalimbali yenye viwango na ukubwa tofauti, aghalabu katika muda mwafaka kwenye eneo la dharura au maafa, kutoa elimu kuhusiana na hali ya tukio pamoja na maagizo yaliyotolewa na mamlaka za udhibiti. Hii itajumuisha mapendekezo ya kuboresha uratibu miongoni mwa wadau mbalimbali kwa kueleza wazi maeneo yanayohitaji kushughulikiwa;

iii Kuweka malengo na muda wa kusambaza mifumo ya Mawasiliano tangamano ya dharura na kupendekeza hatua ambazo watoa huduma za dharura watapaswa kuzizingatia ili kuhakikisha kuna utendajikazi endelelevu wa miundombinu ya Mawasiliano;

iv Kuweka muda ambao kila mdau atatarajia kufikia kiwango cha msingi cha Mawasiliano tangamano ya kitaifa na kuweka vigezo vya kupima maendeleo yake;

v Kupanga majukumu na wajibu kwa ajili ya kuwezesha mfumo wa vitahadharishi vya Mawasiliano pamoja na matengenezo yake ili kuhakikisha kuwa mfumo huo unafanya kazi kwa ufanisi na ubora kabla, wakati na baada ya maafa.

Mpango huu wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura ni sehemu muhimu ya Mpango wa Taifa wa Kusimamia Maafa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Maafa Namba 6 ya 2022. Malengo ya muda mrefu na malengo ya muda mfupi ya NETP hayawezi kufikiwa bila msaada na uratibu wa wadau na timu ya kukabiliana na maafa. NETP utawasaidia wadau kuwa na mkakati wa pamoja wa kukabiliana na changamoto zinazotokana na maafa na majanga ya asili. Hatua zilizopendekezwa katika mpango huu zitasaidia kufikia maono ya pamoja na kutatua changamoto zilizotajwa katika Sera ya TEHAMA ya 2016, kupitia juhudi za pamoja za kuwawezesha watoa huduma za dharura kuwasiliana kama inavyotakiwa kabla, wakati na baada ya maafa au dharura.

## 1. UTANGULIZI

Tanzania kama nchi zingine inakabiliwa na vihatarishi mbalimbali vya asili na vile vinavyotokana na shughuli za kibinadamu. Athari za vihatarishi hivyo zinaweza kuwa na madhara makubwa na hatua stahiki zinahitajika kuchukuliwa ili kuvipunguza. Uwezo wa watu kufanya Mawasiliano yenye ufanisi wakati wa maafa au dharura ni suala la muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama wetu, kwa sababu utapunguza vifo, madhara na athari zingine za kiafya, uharibifu wa mali, njia za uzalishaji mali na huduma, changamoto za kijamii na kiuchumi wakati wa maafa.

Kwa kuzingatia uzoefu wa maafa yaliyotokea hivi karibuni, imebainika wazi kuwa kuna haja ya kuuboresha mfumo uliopo wa Mawasiliano hususani Mawasiliano ya nyakati za maafa au dharura. Suala la kutokuwa na uwezo toshelevu wa Mawasiliano (ya simu, redio na televisheni) na uratibu mzuri wa Mawasiliano hayo ya dharura, limetiliwa mkazo kitaifa kutokana na mfululizo wa matukio mengi yakiwapo yale ya milipuko ya mabomu ya Dar es Salaam ya mwaka 2011 yaliyotokea maeneo ya Gongo la Mboto na Mbagala. Ukosefu wa mpango imara na toshelevu wa Mawasiliano ulisababisha kushindwa kutoa taarifa za tahadhari kwa umma nyakati za maafa.

Kutokana na mambo hayo, Serikali imekuja na Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 ambayo imelenga kuifikia Tanzania iliyo salama, imara na endelevu. Lengo la sera hiyo linaweza kufikiwa kwa kuziwezesha jamii na taasisi ili ziweze kuchukua hatua stahiki za kuzuia na kupunguza vihatarishi na madhara ya maafa ambayo yatapunguza vifo na waathirika, uharibifu wa mali na mazingira.

Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya 2022 inaruhusu uanzishwaji wa Wakala wa Usimamizi wa Maafa, udhibiti wa vihatarishi vya maafa na mbinu za uratibu wa kuzuia, kupunguza, kujiandaa, kukabiliana na kuleta afua baada ya maafa. Idara ya Menejimenti ya Maafa iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ilianzisha Kituo cha Mawasiliano na Utendajikazi wa Dharura (EOCC) chenye Taratibu zake Bora za Utendajikazi (SOPs) ili kuongoza na kusimamia utendajikazi wa saa 24/7.

Jitihada zote hizi zinaelekeza kuwa, pindi maafa yatakapotokea, uratibu mzuri na Mawasiliano madhubuti ni mambo ya muhimu katika kukabiliana na maafa kwa haraka na kwa wakati. Mawasiliano (ya simu, redio na televisheni) yana umuhimu maalumu kwenye kila janga la asili. Kuwapo kwa mfumo mzuri wa Mawasiliano (ya simu, redio na Televisheni), ni jambo lisiloepukika katika kuokoa maisha ya watu nyakati za maafa.

Kama inavyofafanuliwa katika SOP, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imepewa jukumu la kutoa huduma za Mawasiliano na Tahadhari kwa umma. Ni katika muktadha huu kuwa, TCRA inashirikiana na wadau wengine kupanga na kuandaa Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura (NETP) ambao utaisaidia nchi kudhibiti vihatarishi vya maafa.

## 1.1 Madhumuni ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura

Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 nchini Tanzania inahimiza matumizi ya TEHAMA katika kudhibiti maafa kwa kuipa mamlaka Serikali kwanza, kuhakikisha kunakuwapo na mazingira bora kwa ajili ya matumizi bora ya TEHAMA katika kudhibiti maafa na pili, kuimarisha ushirikiano na taasisi husika za kikanda na kimataifa katika kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika udhibiti wa maafa.

Aidha, sera hiyo inadokeza changamoto za TEHAMA katika udhibiti wa maafa, changamoto ambazo ni ukosefu wa mfumo wa kitaifa wa matumizi ya huduma za TEHAMA kwa ajili ya kudhibiti maafa, uwezo mdogo wa kutumia TEHAMA kukabiliana na maafa na upatikanaji mdogo wa njia za Mawasiliano kwa ajili ya utoaji tahadhari za maafa, hususani katika maeneo ya vijijini.

Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura (NETP) ni mpango wa kimkakati ulioandaliwa ili kudhibiti vyema vihatarishi vya maafa wakati wa hatua za kuvipunguza, kufanya maandalizi, kukabiliana navyo na katika hatua za urejeji wa hali kwa kuimarisha Mawasiliano na upashanaji habari kote Serikalini, ndani ya jamii iliyoko kwenye vihatarishi hivyo na kati ya taasisi za umma na binafsi. Udhibiti madhubuti wa maafa hutegemea utoaji wa taarifa kwa wakati na kwa wale wanaouhitaji kadri ya muda unavyokaribia[1].

Kutokana na hayo, mpango huu umeandaliwa ili:

i Kutambua uwezo unaohitajika kwa watoa huduma za dharura ili kuhakikisha kuna utangamano na upatikanaji wa huduma za Mawasiliano kabla, wakati na baada ya dharura na kutambua vikwazo katika usambazaji na matumizi ya mifumo ya Mawasiliano;

ii Kupendekeza usanidi wa mifumo muhimu ya Mawasiliano tangamano inayohitajika kwa watoa huduma za dharura ili kukabiliana nazo kwa ufanisi pamoja na matukio mengine mbalimbali yenye viwango na ukubwa tofauti, aghalabu katika muda mwafaka kwenye eneo la dharura au maafa, kutoa elimu kuhusiana na hali ya tukio pamoja na maagizo yaliyotolewa na mamlaka za udhibiti. Hii itajumuisha mapendekezo ya kuboresha uratibu miongoni mwa wadau mbalimbali kwa kueleza wazi maeneo yanayohitaji kushughulikiwa;

iii Kuweka malengo na muda wa kusambaza mifumo ya Mawasiliano tangamano ya dharura na kupendekeza hatua ambazo watoa huduma za dharura watapaswa kuzizingatia ili kuhakikisha kuna utendajikazi endelelevu wa miundombinu ya Mawasiliano;

---

[1]Global Guidelines to Develop National Emergency Telecommunication Plans, ITU 2019

iv Kuweka muda ambao kila mdau atatarajia kufikia kiwango cha msingi cha Mawasiliano tangamano ya kitaifa na kuweka vigezo vya kupima maendeleo yake;

v Kupanga majukumu na wajibu kwa ajili ya kuwezesha mfumo wa vitahadharishi vya Mawasiliano pamoja na matengenezo yake ili kuhakikisha kuwa mfumo huo unafanya kazi kwa ufanisi na ubora kabla, wakati na baada ya maafa.

## 1.2 Mawanda ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura

Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura (NETP) utashughulikia mahitaji ya Mawasiliano ya dharura nchini katika ngazi zote za Serikali, sekta binafsi na Asasi Zisizokuwa za Kiserikali ili kuhakikisha kuwa, kwa namna yoyote ile kuna uwezekano kwa watoa huduma za dharura kubadilishana taarifa kwa njia ya sauti, data na video pindi dharura au maafa yanapotokea. NETP umelenga kuhakikisha kuwa, wadau wanaweza kuwasiliana kwa njia ya mfumo usiokuwa na changamoto ili kusimamia utoaji huduma za dharura, kutoa maagizo na usimamizi, kutoa elimu kuhusiana na hali ilivyo na kazi inayofanywa na kikundi maalumu cha uokoaji hususani kwenye matukio makubwa. NETP una vipengele vikuu vinne ambavyo ni:

i. **Uwezo wa Utendajikazi** - Uwezo wa watoa huduma za dharura kuanzisha na kuendeleza Mawasiliano katika kuisaidia mifumo ya Mawasiliano.

ii. **Utangamano** - Uwezo wa watoa huduma za dharura kuwasiliana miongoni mwa sekta na ngazi mbalimbali za serikali, kwa kutumia kiwango cha bendi za kujirudia kadri zinavyohitajika na kuidhinishwa.

iii. **Mwendelezo wa Mawasiliano** - Uwezo wa wakala/mashirika yanayotoa huduma za dharura kuendeleza Mawasiliano kwenye matukio ya uharibifu au uvunjifu wa miundombinu mikuu.

iv. **Tahadhari** - Uwezo wa watoa huduma na wadau kuwa na mfumo muhimu wa tahadhari za Mawasiliano yanayohitajika.

## 1.3 Malengo ya Muda Mrefu ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura

Orodha ya malengo maalumu itaandaliwa ili kuwezesha kiwango cha chini kabisa cha Mawasiliano tangamano. Malengo hayo yatadokeza muundo awali wa uendeshaji wa Mawasiliano ya dharura ambao unaweza kuimarishwa zaidi kwa kuwahusisha wadau. Malengo ya muda mrefu ya mpango huu (NETP) ni kama ifuatavyo;

i. Maeneo yote ndani ya nchi yatapaswa kuwa na uwezo wa kupokea tahadhari ya vihatarishi katika vyombo vyote vya habari na Mawasiliano (redio, televisheni,

mitandao ya kijamii na simu) mara tu tahadhari hii itakapotolewa kwenye eneo husika.

ii. Ikitokea miundombinu ya Mawasiliano imeshindwa kufanya kazi kwenye eneo lililoathiriwa, urejeshaji wa huduma za awali utafanyika ndani ya muda usiopungua saa 24.

iii. Watoa huduma za dharura wote na umma watakuwa na uwezo wa kuonesha kiwango cha ushughulikiaji wa matukio ya Mawasiliano ya dharura.

## 1.4 Malengo ya Muda Mfupi ya Mpango wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura

Lengo kuu la la NETP ni kutoa mwongozo utakaoboresha Mawasiliano ya dharura nchini. Ili kufikia azima hiyo, malengo mahususi ya muda mfupi yafuatayo yamepangwa kutekelezwa;

### 1.4.1 Kuandaa na kurasimisha muundo wa kufanya maamuzi ukiwa na majukumu yaliyobainishwa wazi kwa ajili ya kuratibu uwezo wa Mawasiliano ya dharura wakati wa maafa

Wakati wa dharura/maafa, asasi moja au mtu binafsi hawezi kuwajibika kutoa huduma peke yake bila ya kushirikiana na asasi au watu wengine. Kwa hiyo, asasi zote zitahitaji kuwa na njia maalumu zilizopangwa na kuanzishwa ambazo zitatumika ili kuhakikisha kuna huduma nzuri zenye maandalizi yaliyoratibiwa kikamilifu miongoni mwa watu, taasisi na watendajikazi/waendeshaji.

a) Mahitaji & Mapungufu

i. Tukiangalia matukio ya nyuma kama vile milipuko iliyotokea Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam mwaka 2011; wakala wa kukabiliana na dharura hakuwa na uratibu mzuri na asasi zingine ikiwa ni pamoja na waendeshaji mifumo ya Mawasiliano, hali ambayo ilisababisha kuwa na Mawasiliano hafifu miongoni mwa watu na hivyo kuongeza hali ya hofu zaidi. Kwa sasa nchini Tanzania, hakuna mfumo wa Mawasiliano ulioundwa kiotomati kati ya wahusika wakuu/tofautitofauti pindi dharura zinapotokea.

ii. Baadhi ya wadau huwa hawatoi kipaumbele kwenye Mawasiliano na hivyo kuwafanya wasitenge rasilimali zao kwa ajili ya kushiriki katika upangaji wa shughuli.

b) Jitihada za Kushughulikia Mahitaji & Mapungufu

i. Kuwezesha uanzishwaji wa muundo bora wa watoa huduma (serikali, wakala, waendeshaji wa mifumo, watu binafsi na asasi zingine) pamoja na kupanga majukumu maalumu ya Mawasiliano ya dharura ambayo yatabainisha kwa wazi ni nani anayehusika na utoaji wa tahadhari za kitaifa/kimkoa/kiwilaya/kikata na katika ngazi ya kijiji, bila kujali chanzo cha kiashirio cha tahadhari hiyo na taratibu zinazopaswa kufuatwa kwenye ngazi za kijamii/umma kwa njia ya kiotomati.

ii. Kutengeneza sera na miongozo ambayo itakuza ushiriki na uratibu wa watu na vyombo vyote vya habari vinavyohusika katika mchakato wa kupanga, mafunzo ya pamoja, utendaji na usambazaji wa rasilimali kwa ajili ya dharura.

### 1.4.2 Kuimarisha uwezo wa mifumo ya Mawasiliano (Redio, TV, na Mashirika ya Simu za Mkononi kwa kuunganisha na kuboresha mwitikio wa Watoa Huduma za dharura/maafa

Kwa sasa, vyombo vya habari vya Tanzania (TV, redio na mifumo ya mashirika ya simu za mkononi) havijaunganishwa pamoja na njia za Mawasiliano wakati wa maafa, EOCC hakijaunganishwa na vifaa vya Mawasiliano kwa namna ambayo wakati wa maafa au dharura, watoa huduma hawawezi kusambaza kwa haraka taarifa kwa umma, kupitia vyombo hivi vya habari na hivyo kusababisha ucheleweshaji katika usambazaji wa taarifa.

Uboreshaji utapatikana kwa njia ya utekelezaji wa viwango, uundaji, upimaji na tathmini ya mifumo ili nchi iwe na maandalizi ya pamoja ya kupunguza athari, kutoa huduma na kurejesha uwezo wa kuwasiliana wakati wa maafa.

a) Mahitaji & Mapungufu

i. Watoa huduma hawajazihusisha teknolojia za utoaji huduma za dharura kwenye huduma zao za Mawasiliano na hakuna uratibu mzuri uliopo kati ya watoa huduma na EOCC.

ii. Vyombo vya habari kwa umma (redio na TV) vinaweza kutoa taarifa za wakati uliopo lakini taarifa hizo hazitolewi kwa wakati.

b) Jitihada za Kushughulikia Mahitaji & Mapungufu

i. Kuna haja ya kuunda, kupima na kutathmini mfumo wa utatuzi wa changamoto za sauti, video, arafa na data; mfumo ambao utahitaji kujumuishwa katika vifaa vya Mawasiliano ili utumike wakati wa dharura au maafa.

ii. Ofisi ya Waziri Mkuu – Idara ya Menejimenti ya Maafa (PMO –DMD) kuwa na namba mahususi ya dharura na kituo cha simu kinachofanya kazi muda wote

kitakachokuwa kinatoa huduma kwenye matukio yote ya dharura/maafa, huku kikiwasiliana vyema na taasisi zingine zenye wajibu huo.

### 1.4.3 Kuhakikisha kuwa watoa huduma za dharura wanaweza kuwasiliana katika tukio ambalo Mawasiliano ya kawaida yana changamoto

Hili linaweza kuhitaji watendajikazi/waendeshaji kutenganisha mifumo iliyo na hitilafu na kufanya maandalizi ya pamoja, kupunguza athari, kutoa huduma na kurejesha uwezo wa kufanya Mawasiliano wakati wa dharura/maafa. Kuna haja ya kuandaa sera na miongozo ambayo itaongeza uratibu na usambazaji wa rasilimali za miundombinu. Hili litasaidia sana katika mazingira ambayo mwendeshaji mmoja anaposhindwa kufanya kazi, aweze kutumia miundombinu ya mwendeshaji mwingine wakati wa dharura. Zaidi ya hayo, umakini utahitajika katika utoaji wa leseni za Mawasiliano ya simu/TEHAMA au uidhinishaji pindi inapoonekana haja hiyo ili kuunga mkono jitihada za Mawasiliano ya simu/TEHAMA ya dharura.

a) Mahitaji & Mapungufu

i. Udhibiti/usimamizi uliopo wa matumizi ya pamoja ya miundombinu hauhusishi matumizi amilifu ya pamoja ya miundombinu hiyo nyakati za dharura au maafa.

ii. Mfumo uliopo wa utoaji leseni hauruhusu/hautoi nafasi katika utoaji wa leseni za huduma ya Mawasiliano ya simu kwa misingi ya uharaka.

b) Jitihada za Kushughulikia Mahitaji & Mapungufu

i. Kurekebisha kanuni kwenye matumizi ya pamoja ya miundombinu na kuweka masharti ambayo mwendeshaji mmoja anaposhindwa kufanya kazi wakati wa maafa anaweza kuruhusiwa kutumia kikamilifu miundombinu ya mwendeshaji mwingine.

ii. Kuangalia uwezekano wa kuwa na Mfumo wa Kitaifa wa Simu Kutumia Mtandao Mwingine wakati wa dharura/maafa.

iii. Kurahisisha au kuwezesha upatikanaji wa leseni za muda na uidhinishaji wake

- Kuruhusu utaratibu wa utoaji leseni za muda wowote, leseni za muda maalumu na za haraka bila malipo, kwa ajili ya matumizi ya dharura/maafa.
- Leseni zitakuwa za muda na halali hadi pale Serikali itakapoamua kuwa mitandao ya Mawasiliano imerejeshwa katika maeneo yanayohitaji huduma na hakuna haja zaidi ya huduma ya muda/isiyo ya lazima inayotolewa.

iv. Hati/Vibali vyake

- Wakati wa kukabiliana na maafa, mahitaji ya hati/vibali vya vifaa muhimu vya Mawasiliano ya simu/TEHAMA yanaweza kuondolewa.

- Mamlaka za udhibiti zinaweza kutambua vibali vya kigeni ili kuharakisha mchakato ikiwa ni pamoja na kutumia miongozo ya Shirika la Umoja wa Mawasiliano ya Kimataifa (ITU) na Sekta ya Viwango vya Mawasiliano ya Shirika la Umoja wa Mawasiliano ya Kimataifa (ITU-T).

v. Uingizaji wa vifaa

Sheria zinaweza kuwekwa ili:

- Kuweka kipaumbele kwa vifaa vya Mawasiliano vinavyoingia kutokana na umuhimu wake wakati wa kutoa huduma;
- Kuharakisha mchakato wa uingizaji wa vifaa muhimu vya Mawasiliano/TEHAMA kwa ajili ya kutolea huduma za maafa;
- Misamaha ya ushuru na kodi, iweke wazi michakato ya haraka na nyaraka zinazofanyiwa kazi;
- Kuwa na taratibu za haraka zinazoruhusu vifaa kurudishwa mahali vilipotoka.

### 1.4.4 Kutoa mafunzo ya kutosha, endelevu na vipindi vya mafunzo ya dharura kwa vitendo

Watoa huduma za dharura, mashirika na watoa huduma za kawaida watahitaji kufanya mafunzo pamoja na kuvijaribisha vifaa vyao mara kwa mara na kujua namna ya kuviendesha wakati wa dharura ili wote waweze kuwa na mbinu/uelewa wa pamoja, huduma zilizoimarishwa na uwezo mahiri wa kiutaalamu. Mafunzo ya kawaida na mafunzo kwa vitendo yana umuhimu mkubwa sana katika maandalizi, utayari na ustadi katika kupata na kutumia vifaa vya Mawasiliano wakati wa matukio ya dharura.

a) Mahitaji & Mapungufu

Kuna haja ya kuwa na mafunzo kamili ya vitendo/mazoezi mengi ya kurudiarudia yatakayoratibiwa kwa wahusika wote wa kutoa huduma za dharura.

a) Jitihada za Kushughulikia Mahitaji & Mapungufu

Mpango utaanzishwa kwa ajili ya kuendeleza mafunzo na mafunzo fananivu ya vitendo ili kutoa maarifa yanayofaa kwa watoa hudumu na wahusika wote wa dharura. Hili litawajengea uwezo na uelewa katika kukabiliana na matukio ya dharura.

### 1.4.5 Ushirikiano wa Kimataifa

Nchi inahitaji kuutumia mfumo uliopo wa Mashirika ya Kimataifa kama vile ITU kwa masuala yanayohusiana na maafa.

Mpangilio maalumu wa masafa ya mawimbi ya redio ni kipengele muhimu katika mpango wowote wa kitaifa wa kudhibiti maafa.

Katika ngazi ya kikanda, nchi wanachama wa Chama cha Wasimamizi wa Mawasiliano Kusini mwa Afrika (CRASA) waliona haja ya kuyawianisha masafa hayo kupitia bendi za masafa sahihi ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ili kushughulikia mahitaji ya Sekta ya Ulinzi wa Watu/Umma na Misaada ya Maafa (PPDR). Mfumo uliowianishwa wa SADC wa masafa ya redio kwa PPDR umeanzishwa ili kuziruhusu nchi wanachama wa SADC ziweze kusaidiana zenyewe wakati wa maafa kama haya kwa misingi na uratibu uliopangwa.

a) Mahitaji & Mapungufu

i . Tanzania bado haijaridhia Mkataba wa Tampere. Kuridhiwa kwa mkataba huo wa Tampere:

a) Kutawezesha matumizi makubwa ya vifaa vya Mawasiliano ya nchi kavu na satelaiti ili kutabiri, kufuatilia na kukabiliana na maafa makubwa duniani kote;

b) Kutatoa utaratibu ndani ya Shirika la Kimataifa la Umoja wa Mawasialiano katika utoaji misaada ya Maafa kwa ajili ya usambazaji wa kimataifa wa vifaa vya Mawasiliano, wafanyakazi na uratibu wa jitihada za kutoa misaada ya maafa; na

c) Kutapunguza vikwazo vya udhibiti, kama vile taratibu za upatikanaji wa vibali vya forodha na sheria za ulinzi wa data, kwa ajili ya usambazaji wa haraka wa taarifa na matumizi ya vifaa umuhimu vya Mawasiliano kwa ajili ya udhibiti wa maafa.

ii. Uorodheshaji wa vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kutoa misaada ya maafa.


b) Jitihada za Kushughulikia Mahitaji & Mapungufu

i. Serikali ya Tanzania kuusoma na kuuridhia mkataba wa Tampere kwa kuingiza masharti yake yaliyopo kwenye sheria na kanuni husika za kitaifa za Mawasiliano/TEHAMA.

ii. Kuchukua hisa za vifaa vinavyohitajika na kuanzisha mfumo utakaohakikisha kuwa vifaa vilivyotengwa kutumika wakati wa maafa, vinaendana na bendi ya PPDR.

## 2. NAFASI YA MAWASILIANO KATIKA KUDHIBITI MAAFA

Mchakato wa Kudhibiti Maafa una awamu nne[2] za upunguzaji, maandalizi, utoaji wa huduma na misaada (uitikiaji), urejeshaji na ukarabati kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 1**. Mawasiliano ya simu ni muhimu katika awamu zote za udhibiti wa maafa. Sura hii inaelezea umuhimu wa Mawasiliano/TEHAMA katika kila awamu wakati wa kudhibiti na kupunguza vihatarishi vya maafa.




*Kielelezo cha 1: Awamu za Kudhibiti Maafa[3]*

### 2.1 Matumizi ya Mawasiliano katika Kupunguza Maafa

Awamu hii inahusisha shughuli zinazolenga kuzuia maafa au dharura, kupunguza uwezekano wa kutokea kwake au kuzuia athari mbaya za matishio yanayoepukika. Shughuli hizi ni hatua za muda mfupi na za muda mrefu za sekta mbalimbali ili kulinda maisha ya watu na kushusha au kupunguza uharibifu unaoweza kusababishwa na maafa au hali ya dharura.

Shughuli hizi zinajumuisha;

a) Kufanya maandalizi kwa ajili ya majanga ya asili yaliyoarifiwa kabla na kukagua maeneo hatarishi ya ndani/yenye historia mbaya,

b) Kufanya uchambuzi wa mazingira hatarishi ya miundombinu muhimu ya Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA;

---

[2]The disaster risk management process adopted internationally by United Nations Office for Disaster Risk Reduction (UNDRR) consists of these four phases. See European Commission, United Nations Development Group and World Bank (2013)

c) Kufanya maboresho thabiti katika mitandao ya Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA;
d) Kufanya maandalizi ya mfumo wa kisheria na udhibiti ili kusaidia kutoa huduma za dharura za Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA kwa mf. kanuni na miongozo;
e) Kuweka rasilimalifedha; na
f) Kuanzisha Ubia kati ya Sekta za Umma na Binafsi

### 2.1.1 Muhtasari wa Maafa nchini Tanzania

Kwa ujumla, maafa hufafanuliwa kama tukio lisilotarajiwa ambalo husababisha uharibifu, maangamizi na mateso makubwa ya kibinadamu ambayo yako nje ya uwezo wake na hivyo kuhitaji msaada wa nje katika ngazi ya kitaifa au kimataifa.


Maafa yanaweza kubainishwa katika makundi makuu matatu: maafa ya asili, maafa ya kiteknolojia na maafa yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu.


Kwanza, maafa ya asili yamegawanyika katika makundi madogo matatu yaani maafa ya Hali ya Hewa inayotokana na maji yakiwamo mafuriko, dhoruba, ukame, tufani za upepo, maporomoko ya ardhi na mtiririko wa matope; Maafa ya kijiofizikia yakiwamo matetemeko ya ardhi, tsunami na milipuko ya volkeno na maafa ya Kibiolojia kama vile magonjwa tandavu (k.v. UVIKO 19), magonjwa ya mlipuko (k.v. Kipindupindu), mashambulizi ya wadudu na wanyamapori/mimea;

Pili, maafa ya kiteknolojia yanayogawanyika katika vikundi viwili vidogovidogo: (1) ajali za viwandani kama vile kumwagika kwa kemikali, kuharibika kwa miundombinu ya viwandani, mioto na mionzi na (2) ajali za usafiri wa anga, reli, barabara au majini.

Mwisho, maafa yanayotokana na shughuli za kibinadamu ambayo yamegawanyika katika makundi mawili madogomadogo: (1) migogoro ya kiuchumi inayohusisha mfumuko mkubwa wa bei na mgogoro wa kifedha na/au sarafu na (2) vurugu kama vile ugaidi, mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, ghasia na vita na hivyo kuhitaji msaada wa kimataifa. Hata hivyo, Tanzania imekuwa ikikumbwa zaidi na maafa ya asili.

Kielelezo cha 2 hapa chini kinatoa idadi ya majanga ya asili kulingana na aina zake kwa miongo miwili iliyopita kuanzia 1997 hadi 2017 nchini Tanzania. Takwimu zinaonesha kuwa, idadi kubwa ya vifo vilitokana na majanga ya milipuko ya maradhi ambayo ilichangia takriban 92% ya vifo vyote vilivyosababishwa na majanga. Kwa upande mwingine, ukame uliathiri idadi kubwa ya watu ambapo 91% ya waathirika zilitokana na ukame.




**Hali ya tabia ya nchi iliyopo 1997 - 2018) conditions (1979**

**Mipango ya kijamii na kiuchumi (2051 – 2100)**

*Kielelezo cha 2: Utokeaji wa maafa ya asili kwa aina zake nchini Tanzania katika miongo miwili iliyopita kuanzia 1997 hadi 2017*

**(Chanzo: PMO, UNDRR na CIMA, 2019)**

Tanzania imeorodheshwa kuwa ni nchi ya 51 kati ya nchi 180 duniani zilizoko kwenye hatari ya kukumbwa na maafa ya asili. Jumla ya idadi ya watu ni takriban milioni 61.7[3], kutokana na kiwango cha ongezeko la watu la takribani asilimia tatu. Kwa mujibu wa Fahirisi ya Kuendana na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi (*Notre Dame-Global Adaptation Index (ND-GAIN)*), Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo hazina maandalizi ya kutosha kukabiliana na maafa ya asili. Iko katika nafasi ya 138 kati ya nchi 182 kutokana

[3]https://sensa.nbs.go.tz/

na kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na uharibifu wa tabia ya nchi (2016). Nchi hii iko kwenye nafasi ya 145 kati ya nchi 182 zenye uwezo wa kuendana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Ina uwezo mdogo wa ushawishi na kubadilisha uwekezaji kuwa katika vitendo vya kuendana na mabadiliko hayo, kama inavyothibitishwa na nafasi yake ya 153 kati ya nchi 192 zenye utayari huo.[4]

### 2.1.2 Uchambuzi wa Vihatarishi vya Miundombinu ya Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA

Kuitambua miundombinu yote muhimu ya Mawasiliano ya simu/vifaa/TEHAMA ambayo vinaweza kuathiriwa na maafa ya asili, mafuriko, kukumbwa na vimbunga na kisha kuchukua hatua zinazoweza kusaidia katika kuzuia uharibifu wa miundombinu ya Mawasiliano wakati wa maafa.

### 2.1.3 Kupunguza Athari na Kuimarisha Uthabiti wa Mitandao ya Mawasiliano ya Simu za mkononi/TEHAMA

Kuhakikisha kuwa, mitandao yote ya Mawasiliano ya simu/TEHAMA haiathiriwi na maafa ya asili kadri inavyowezekana na kuweka orodha ya vifaa vya kuhifadhi taarifa zinazoweza kutumiwa na miongoni mwa watoa huduma na ambazo pia zinaweza kutumika endapo kutakuwa na kufeli kwa mitandao.

### 2.1.4 Mfumo wa Kisheria na Udhibiti

Ili Kupunguza Maafa kwa ufanisi, Mfumo wa Kisheria na Udhibiti unaokubalika unahitajika. Mfumo huo utapaswa uruhusu hali ya mabadiliko ili kusaidia uendeshaji endelevu na urejeshaji wa miundombinu ya Mawasiliano. Aidha, Mfumo wa udhibiti utapaswa uruhusu Mawasiliano/TEHAMA na vyombo vya utangazaji kufanya kazi zake katika usambazaji wa taarifa ili kupunguza athari za maafa.

#### A. Utoaji Leseni za Huduma ya Mawasiliano /TEHEMA

Ili kuwa na hali ya mabadiliko (unyumbufu) katika utoaji wa leseni za huduma ya Mawasiliano na TEHAMA na kwa kuzingatia uharaka, mf. matumizi ya leseni za mpangilio wa masafa mafupi na uwekaji namba za vifaa/rasilimali, usanidi na leseni za matengenezo ya vifaa vya Mawasiliano ya kielektroni au vibali pale itakapohitajika kusaidia jitihada za kuwezesha Mawasiliano ya dharura. Taratibu za kipekee za utoaji wa leseni za haraka zitapaswa kuwapo kwa ajili ya matumizi katika mazingira ya dharura/maafa, leseni hizo zitakuwa za muda na halali kwa kipindi cha kukabiliana na maafa na kurejesha afua hadi pale Serikali itakapotamka kuwa hakuna haja tena ya kuendelea kutoa huduma zilizokuwa zinatolewa.

[4]https://gain.nd.edu/our-work/country-index/rankings/

**B. Uwekaji wa Mpangilio wa Mawimbi ya Redio, Usambazaji na Uidhinishaji**

Uwekaji wa mpangilio wa mawimbi na usambazaji ni mambo ya msingi sana katika awamu zote nne za udhibiti wa maafa/dharura. Uwekaji wa mpagilio wa mawimbi (RF) utahitaji kuwapo kwa mifumo midogo na mikubwa ya bendi lakini pia kwa ajili ya maendeleo ya haraka ya mitandao ya Mawasiliano ya bendi kubwa za redio.

Mitandao ya Mawasiliano ya bendi kubwa za redio huwezesha upatikanaji wa programutumizi za bendi mahiri/kubwa kwa watoa huduma wa mwanzo mf. kurusha matangazo mbashara ya video, uwezo mkubwa wa vyombo vya habari na usahihi wa taarifa na mwonekano mzuri wa picha na mazingira. TCRA imeweka mpangilio wa masafa kwa PPDR kwa ajili ya watoa huduma za usalama kwa umma kuutumia wakati na mahali utakapohitajika kwa misingi ya kitaifa ambayo itawezesha aina nyingi za programutumizi na huduma kama vile sauti, picha zilizopunguzwa ukubwa au picha, upatikanaji wa kanzidata, kamsa/vitahadharishi, eneo/ufuatiliaji na urushaji wa matangazo mbashara ya video kutoka kwenye huduma za sauti za bendi ndogo kwenda kwenye programutumizi za bendi mahiri/kubwa.

Orodha ya mawimbi ambayo yametolewa kama sehemu ya Mpango wa Taifa wa Uwekaji wa Mawimbi imeoneshwa katika Jedwali la 2.

Jedwali la 2: Uwekaji wa Mawimbi ya Dharura

| Mawimbi | Uwekaji |
|---|---|
| 380-385 MHz yamewekwa sambamba na 390 -395 MHz | Bendi ndogo PPDR na Bendi kubwa PPDR |

**C. Matumizi ya Pamoja ya Miundombinu**

Kuruhusu matumizi amilifu ya pamoja ya miundombinu au Mfumo wa Taifa wa Simu Kutumia Mtandao Mwingine kutawawezesha waendeshaji kutumia kila mmoja vifaa/rasilimali za mwenzake hususani wakati changamoto inapotokea kwenye baadhi ya viungo vya Mawasiliano.

## 2.2 TEHAMA/Mawasiliano ya Simu katika Awamu ya Maandalizi ya Maafa

Awamu hii itahusisha hatua zinazochukuliwa ili kuimarisha uwezo wa watu binafsi, jumuiya, timu za watoa huduma na wafanyabiashara kukabiliana na maafa/dharura. Aidha, awamu hii itahusisha kujenga uwezo wa kudhibiti dharura ili kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kupunguza, kukabiliana na kuleta afua zinazotokana na janga lolote kwa kupanga, kutoa mafunzo na kufanya mazoezi kwa vitendo.

Katika NETP huu, Maandalizi ya Maafa yana maana ya hatua zinazochukuliwa kujiandaa na kupunguza athari za maafa kwa lengo la kuokoa maisha ya watu wengi, uharibifu wa mali pamoja na njia zao za uzalishaji mali wakati wa maafa yoyote, ili kuwawezesha Watanzania walioathiriwa kurejea katika hali zao za kawaida ndani ya muda mfupi. Shughuli za maandalizi kwa kuzingatia Mawasiliano zitahusisha;

a) Utekelezaji wa NETP;
b) Uaandaaji wa Taratibu Bora za Utendajikazi (SOP);
c) Utekelezaji wa Mifumo ya Tahadhari za Mwanzo;
d) Kujenga uwezo na kutoa mafunzo kwa vitendo; na
e) Kushirikishana taarifa na maarifa;
f) Utekelezaji na matumizi ya teknolojia mpya;
g) Maandalizi ya kurejesha nguvu/nishati na vifaa;
h) Utekelezaji wa mifumo ya kuleta afua za maafa; na
i) Matumizi ya picha za satelaiti.

### 2.2.1 Mfumo wa TEHAMA wa Kukabiliana na Maafa

TEHAMA kupitia utangazaji (redio, televisheni), Mawasiliano ya simu, intaneti, mawimbi makubwa sana (VHF) na mifumo ya Mawasiliano ya satelaiti (mf. Kituo Kidogo Sana Kinachopitisha Mawimbi ya Data, Sauti na Video za Satelaiti (VSAT)) ina kazi kubwa katika kuelimisha umma kuhusiana na vihatarishi vya maafa yanayoweza kutokea au yanayokuja.


TEHEMA inaweza kutumika kwa kutahadharisha maafa ya kabla kwa kusambaza taarifa kuhusiana na hatari inayokuja na hivyo kufanya uwezekano wa kuchukua tahadhari zinazohitajika ili kupunguza athari za maafa hayo.

TCRA itatoa uratibu miongoni mwa waendeshaji na Kituo cha Uendeshaji na Mawasiliano ya Dharura (EOCC) na kukiunganisha na waendeshaji wapya.

Mara tu ujumbe wa tahadhari utakapoandaliwa na Mamlaka iliyoidhinishwa na kutumwa kwenda kwenye EOCC; EOCC itautuma ujumbe huo kwenda kwenye vituo vya Televisheni na Redio vinavyofanya kazi katika eneo lililoathiriwa kulingana na ukubwa wa maafa. Aidha, ujumbe uleule utatumwa kwa waendeshaji wa Simu ambao watasambaza ujumbe unaowatahadharisha watu kuhusiana na maafa. Kuna njia mbili kuu za kutuma ujumbe kwa umma: kwa kutumia matangazo ya simu au huduma za ARAFA (SMS) kwa watumiaji wa simu/washitariki waliokusudiwa.

Umma unaweza kukiarifu EOCC kuhusiana na maafa yoyote yanayoanza au yanayotokea kupitia namba maalum, iliyotangazwa kwa umma ili itumike wakati wa dharura.

Mchoro wa kiwango cha juu unaoonesha namna TEHAMA inavyoweza kuwa mwezeshaji katika uendeshaji wa EOCC na kuwezesha mtiririko wa taarifa kati ya taasisi zinazohusika kupunguza maafa, ambao umeoneshwa kwenye Kielelezo cha 4.




*Kielelezo cha 4: Mfumo wa Taarifa za Kukabili Maafa*

### 2.2.2 Kuwa na Mfumo wa Simu Hawilishi za Kipaumbele

Wakati wa majanga/dharura, mitandao inaweza kushindwa kutoa huduma kwa sababu mbalimbali: mf. kukatika kwa umeme, kuharibika kwa miundombinu, mitandao kuwa na watumiaji kupita kiasi na sababu zinginezo. Kwa hiyo, mitandao huwa na misongamano, huchelewesha au kuzuia kabisa Mawasiliano muhimu kati ya watoa huduma wa kwanza na jamii iliyoko kwenye mazingira hatarishi. Utaratibu utawekwa ili kuruhusu uanzishaji wa mfumo wa kuwa na simu za kipaumbele kwenye simu na mitandao isiyoingiliana/badilika kwa ajili ya watu wanaojihusisha katika shughuli za utoaji wa huduma na afua wakati wa maafa/dharura pamoja na taasisi zingine zinazojihusisha na shughuli hizo.

### 2.2.3 Vifaa na Namba za Dharura

TCRA imepanga na kujiwekea mfumo wa huduma za kimaisha na kiusalama kwa wananchi; huduma ambazo zitakuwa ni za bure. Watoa huduma za simu na wa mitandao isiyoingiliana watapaswa kuutekeleza uhawilishaji wa namba hizi za simu ili zitumike wakati wa maafa/dharura.

Namba ya dharura zilizotengwa kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Utoaji wa Namba kufikia Julai 2022 zimeoneshwa kwenye Jedwali la 3.

Jedwali la 3: Utoaji wa Namba kwa ajili ya Huduma za Dharura

| NA. | KIWANGO CHA 11X &19X | MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1. | 110 | Huduma za dharura kwenye Ziwa Victoria na vyanzo vingine vya maji |
| 2. | 111 | Wazuia/Wadhibiti Uhalifu |
| 3. | 112 | Dharura, Polisi |
| 4. | 113 | Kupambana na Rushwa |
| 5. | 114 | Huduma za zimamoto na uokoaji |
| 6. | 115 | Huduma za gari la wagonjwa |
| 7. | 116 | Namba ya msaada kwa watoto |
| 8. | 117 | Namba ya msaada wa kiafya |
| 9. | 119 | Kupambana na Madawa ya Kulevya |
| 10. | 190 | Huduma za maafa |
| 11. | 199 | Dharura ya Mlipuko wa Magonjwa |

Wakati wa kutoa huduma na afua za maafa, mahitaji ya Kibali kwa ajili ya vifaa muhimu vya Mawasiliano/TEHAMA, hayana budi kuharakishwa. TCRA itaharakisha mchakato wa kutoa Kibali kwa ajili ya vifaa vya Mawasiliano vilivyoingia nchini wakati wa maafa/dharura.

### 2.2.4 Vitahadharishi Awali na Mifumo Inayohamasisha

Vitahadharishi awali na mifumo inayohamasisha ni mifumo jumuishi ya ufuatiliaji wa hatari, utabiri na ubashiri wa hatari, tathmini ya vihatarishi vya maafa, shughuli za Mawasiliano na maandalizi, mifumo na michakato ambayo itawawezesha watu binafsi, jamii, serikali, wafanyabiashara na watu wengine kuchukua hatua kwa wakati ili kupunguza vihatarishi vya maafa kabla ya kutokea kwa matukio ya majanga hatarishi.

Mifumo ya tahadhari za kabla itawahusu watu na itagawanywa katika makundi yafuatayo:

a) Uelewa kuhusiana na vihatarishi vya maafa

Watu walioko hatarini watapaswa kuzielewa hatari kubwa na viashirio vyake vyote vilivyobainishwa katika eneo/mkoa husika. Aidha, jukumu na wajibu wa wadau wote utatekelezwa na taarifa za hatari zitaunganishwa na kuwasilishwa kwa umma wote ili uzielewe.

b) Ugunduzi, ufuatiliaji, utabiri na uchambuzi wa hatari na athari zinazoweza kujitokeza

Mifumo ya ugunduzi, ufuatiliaji, na utoaji wa tahadhari itapaswa kuwapo na inayofanya kazi. Aidha, kutakuwa na mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uchambuzi wa kila siku wa majanga yanayofuatiliwa na kugundulika.

c) Usambazaji wa Tahadhari na Mawasiliano

Mifumo ya Mawasiliano na vifaa vya kutoa tahadhari za kabla, vitakuwapo kwa ajili ya usambazaji mzuri wa taarifa kwa kundi lengwa. Mfumo wa Tahadhari za Kabla (EWS) utatumia huduma zote za nchi kavu na satelaiti kufuatilia maafa yanayoweza kujitokeza na kisha kutoa tahadhari na vitahadharishi sahihi na kwa wakati. EWS umegawanyika katika makundi yafuatayo:

i. Huduma ya utangazaji yaani Redio, redio za Ridhaa na utangazaji wa TV ambao utatahadharisha maafa yanayokuja.
ii. Huduma za simu: zitasambaza taarifa kupitia utangazaji wa simu za mkononi kama vile kutuma ujumbe mfupi kwa sababu ujumbe huu utafanya kazi bila ya taarifa za kupiga simu ambapo utafika kwa wakati huohuo kwenye vituo vingi vya simu ndani ya eneo la maafa.
iii. Aina zingine za mifumo ya tahadhari.
    a. Mifumo ya anwani za umma (PA) itaunganishwa kwenye vitambuzi ambavyo vitapiga kengele pindi kiwango mahususi cha tahadhari kitakapofikiwa. Mifano ya mifumo hii ni ving'ora na mifumo ya PA iliyowekwa kwenye maeneo hatarishi.

### 2.2.5 Utumaji wa Arafa kwa ajili ya Tahadhari kwa Umma

Utumaji wa Arafa (*Cell Broadcast*) ni huduma ya kawaida ya Mawasiliano ya simu za mkononi ambayo huwezesha kutuma ujumbe mfupi kutoka kwenye minara ya simu kwenda kwa watumiaji wote wa simu za mkononi katika eneo husika. Huduma hii huwezesha ujumbe kutumwa na kupokelewa mara moja kwa watumiaji wote na hivyo kuwa ni njia bora ya kutoa tahadhari kwa umma katika tukio la dharura inayotishia maisha ya watu. Huduma hii ina faida kadhaa[5]:

a) Hutuma ujumbe kwa wachache au mamilioni ya watu ndani ya sekunde 10;
b) Husaidia toni ya mlio maalumu na uliotengwa na mtetemo;


[5]https://en.wikipedia.org/wiki/Cell_Broadcast

c) Ipo kwenye 99% ya simu zote zinazotumiwa leo;
d) Hutumia lugha nyingi, huviwezesha viungofora (*hyperlinks*) kwenye kitahadharishi;
e) Huwafikia washtariki wote ikiwa ni pamoja na simu kutumia mitandao mingine;
f) Huwafikia washatariki wote katika lugha zao;
g) Haiathiriwi na msongamano wa mtandao wa simu;
h) Haiathiriwi na vizuizi/vikwazo vya utunzaji wa data;
i) Inaweza kuwafikia watu katika mtaa mmoja au mitaa yote ndani ya jiji au nchi;
j) Inafaa kwa majaribio ya mara kwa mara ya uelewa wa tahadhari kwa umma;
k) Ina matumizi madogo ya nishati ya betri ya simu za mikononi.

### 2.2.6 Protokali Jumuishi ya Kutahadharisha (CAP)[6]

Protokali Jumuishi ya Kutahadharisha (CAP) ni muundo wa kidijiti wa kubadilishana vitahadharishi na tahadhari za dharura kwa umma kwenye aina yoyote ya mtandao. CAP huwezesha ujumbe wa tahadhari kutangazwa kwa wakati mmoja kwenye mifumo tofautitofauti ya tahadhari na hivyo kuongeza ufanisi wa kutahadharisha na kuirahisisha kazi ya kuitangaza tahadhari hiyo. Aidha, CAP hutoa kiolezo cha ujumbe wa tahadhari yenye ufanisi, kutokana na mbinu bora zilizotambuliwa katika utafiti wa kitaaluma na katika uzoefu halisi wa kimaisha.

CAP ni lazima itatue/ikabiliane na changamoto na siyo tu kwa kutoa vitahadharishi sahihi kwa wakati bali pia kwa kuhakikisha kuwa vitahadharishi hivyo vinawafikia wale tu wanaovihitaji. CAP itamwezesha mtumaji kutuma arafa nyingi za tahadhari kwa mkupuo mmoja. Jambo hili litaiwezesha tahadhari ya CAP kuwafikia watumiaji kwa njia ya miundo mingi kama vile Simu za Mkononi, Simu za mezani, intaneti (baruapepe, mitandao ya kijamii kama vile Facebook, twitter na WhatsApp, Intanet ya vifaa/maunzi magumu ya kompyuta), ving'ora, matangazo ya televisheni na redio, televisheni ya kebo, matangazo ya moja kwa moja ya setilaiti na mitandao ya alama za kidijiti (ishara za barabara kuu na mabango). Kielelezo cha 5 kinaielezea CAP.




[6]Recommendations ITU-T X.1303

*Kielelezo cha 5: Protokali Jumuishi ya Kutahadharisha*[7]

Data hizo za eneo linalotahadharishwa zitaziwezesha kwa namna zote zanamango (*internet of things devices*) za Mawasiliano/TEHAMA kuifikisha tahahari iliyokusudiwa kwa watu walioko katika mazingira hatarishi[8]:

a) Simu za mkononi zitapata vitahadharishi vya CAP kupitia ARAFA au utumaji wa arafa hizo kwa simu.
b) Watumiaji wa mtandaoni watapata vitahadharishi vya CAP kiotomati ikiwa wanatumia huduma ya mtandaoni wa Google.
c) Ving'ora na vifaa vya nyumbani vitatoa vitahadharishi vya CAP kwa sauti kubwa.
d) Redio na televisheni zitabeba kiotomati vitahadharishi vya CAP kama maandishi ya chini ya skrini au viingizo/vichochezi vya sauti.
e) Baadhi ya watumiaji wa mtandaoni watapata vitahadharishi vya CAP kama safu ya matangazo ya mtandaoni.
f) Madereva watavиona vitahadharishi vya CAP kwenye mabango ya kidijiti kando ya barabara kuu.
g) Simujanja zitapata vitahadharishi vya CAP kupitia programutumizi zisizolipiwa kama vile Programutumizi ya *Red Cross Hazard*, ambayo huwa na taarifa zaidi, kama vile mahali pa kupata malazi/makazi na jinsi ya kutoa huduma ya kwanza.

### 2.2.7 Uwezo wa Kufanya Maandalizi ya Kukabiliana na Maafa

Sehemu hii itahakikisha kuwa hatua za kufanya maandalizi kwa ajili ya maafa kama vile mipango ya kukabiliana nayo, imeanzishwa na inafanya kazi. Aidha, kampeni za uhamasishaji na utoaji elimu kwa umma zitafanyika.

a) Mipango ya Dharura

Kuna haja ya kufanya maandalizi zaidi ya taratibu za uendeshaji na mipango ya kuwezesha huduma za Mawasiliano katika baadhi ya maeneo ambayo yamekumbwa na maafa ili kusaidia kuendelea kufanya kazi na kurejesha Mawasiliano. Mpango huo utatokana na topolojia ya uchambuzi wa maafa na utabainisha kutokuwapo kwa miundombinu ya Mawasiliano/TEHAMA katika maeneo hatarishi kama vile uunganishwaji wa kabla kwenye eneo, kuwapo kwa vifaa vya Mawasiliano/TEHAMA na vifaa vya Mawasiliano vilivyoandaliwa ambavyo vinaweza kupelekwa katika maeneo yenye vihatarishi vya kukumbwa

[7] ITU
[8] ITU Guidelines for national emergency telecommunication plans, 2019

na maafa. Kila mtoa huduma za Mawasiliano atahitaji kuwa na mpango wa dharura ambao utakuwa na hatua mahususi kama vile;

i. Kiwango cha uunganishwaji wa kabla kwenye eneo
ii. Vifaa vya uendeshaji/kuwapo kwa vifaa vya Mawasiliano/TEHAMA
iii. Vifaa vilivyowekwa kabla ambavyo vinaweza kusambazwa katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na:
   - Kukatika kwa umeme: jenereta za maeneo husika na vyanzo vya kurejesha nishati na kusambaza jenereta rahisi/nyepesi.
   - Kuepuka msongamano wa kusimamia ufuatiliaji wa mtandao kama utahitajika.
   - Minara Inayotembea (COW) – minara ya simu za mkononi.
   - Kuhifadhi vituo vya satelaiti (kama vile VSAT) kwenye maghala salama tayari kwa kuvisambaza.

b) Mtandao wa Ziada

Kuwa na mitandao thabiti ili kupunguza kukatika kwa Mawasiliano/TEHAMA wakati wa dharura/maafa, ubadala na uziada wake ni mambo ya muhimu kuyazingatia. Lengo ni kuwa na mipango ambayo itawahamasisha watoa huduma za Mawasiliano/TEHAMA kuwa na mitandao yenye uziada wa kutosha na yenye njia nyingi za kuunganishia.

### 2.2.8 Mipango ya Kukabiliana na Dharura

Mpango wa dharura ni mlolongo wa majadiliano, uchambuzi na uamuzi muhimu zaidi unaofanywa wakati wa mchakato wa kupanga, pia ni njia ya kuwasilisha mawazo haya kwa watu ambao wanaweza kuhusika katika mchakato wa kupanga. Jedwali la 4 linaonesha uchambuzi wa mpango wa kukabiliana na dharura.

Jedwali la 4: Mipango ya Kukabiliana na Dharura

| Na. | Kipengele cha mpango wa dharura | Matumizi makuu |
|---|---|---|
| 1 | Mpangilio | ▪ Kutoa sababu za kuwa na mpango<br>▪ Utatumika katika ufumbuzi wa changamoto nyingi za vizazi vitakavyokuwa kwenye matatizo ya aina hii |
| 2 | Mkakati wa kukabiliana | Kuanzisha huduma sahihi za kibinadamu |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Mpango wa Utekelezaji | Kufafanua jinsi huduma hizo zitakavyokuwa na zitakavyotekelezwa katika programu na mtiririko maalumu. |
| 4 | Mpango wa kusaidia uendeshaji | Kutambua rasilimaliwatu, utawala, fedha, Mawasiliano/TEHAMA, usalama na mahitaji mengine ya huduma. |
| 5 | Mpango wa maandalizi | Kutambua hatua zinazoweza kuchukuliwa kabla ya maafa ili kuboresha utoaji wa huduma |
| 6 | Bajeti | Kubainisha gharama ya shughuli za maandalizi na utoaji wa huduma |

### 2.2.9 Mitandao ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi/TEHAMA kwa ajili ya Ufuatiliaji wa Mifumo ya Tahadhari na Vitahadharishi vya mwanzo

Tengeneza mfumo wa Tahadhari ya Mwanzo wenye mtiririko mzuri wa taarifa na Mawasiliano; andaa na sambaza miongozo ya mwitikio wa Tahadhari ya Mwanzo kuanzia ngazi ya juu kitaifa hadi ngazi ya mtaa/kijiji

.

### 2.2.10 Mawasiliano ya Simu za Mkononi/TEHAMA katika Udhibiti wa Maafa na Upunguzaji wa Vihatarishi

Idara ya Menejimenti ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu (DMD - OWM) itahitaji kujipanga ikihusisha Mawasiliano/TEHAMA katika hatua zote za mfumo wa maisha ya kukabiliana na maafa, hususani katika hatua ya maandalizi.DMD - OWM, Wizara yenye dhamana ya Mawasiliano, TCRA na wadau wengine muhimu watatakiwa kuongeza jitihada katika kuendelea kuimarisha miundombinu ya Mawasiliano nchini ili iwe na ufanisi katika kuokoa maisha ya watu na mali pindi maafa yanapotokea. Mawasiliano/TEHAMA vitatumika katika eneo lifuatalo wakati wa udhibiti wa vihatarishi vya maafa ili kuhakikisha kuwa wadau mbalimbali wanashiriki katika kuandaa, kuhuisha na kupashana habari kuhusiana na Upunguzaji wa Vihatarishi vya Maafa kwa:

a) Kuweka mifumo ya tahadhari na vitahadharishi vya maafa.
b) Kutengeneza kanzidata kwa ajili ya usambazaji wa taarifa.
c) Kutengeneza ramani za Mfumo wa Taarifa za Kijiografia za maafa na vihatarishi vya kitaifa.
d) Kutengeneza vifaa vinavyotathmini hatari zilizopo na zinazoweza kusababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa jamii zilizopo kwenye mazingira hatarishi nchini Tanzania.
e) Kutengeneza mfumo wa kitaifa wa tahadhari za mwanzo, sensa na vitahadharishi vya dharura ili kuwashauri wadau wote wa udhibiti wa maafa.

f) Kuunda majukwaa ya Mawasiliano/TEHAMA ambayo yataziunganisha taasisi na mifumo ya tahadhari za mapema itakayowekwa kwenye maeneo yaliyoko kwenye hatari zaidi.
g) Kutengeneza Mfumo wa Kitaifa wa Kutuma Arafa za Simu kwa Umma ambao utawezesha kutuma ujumbe wa taarifa kwa wakati ndani ya eneo mahususi kwa idadi kubwa ya watumiaji wa huduma za Mawasiliano ya simu.
h) Kuanzisha Kituo cha Utendajikazi wa Kiintelijensia (IOC) chenye vifaa vya kiotomati vya Mawasiliano ya dharura ili kukabiliana na maafa.
i) Kutumia Ndege Zisizokuwa na Rubani (UAV) ili kutoa taarifa kutokana na picha/taswira za mwonekano wa angani kuhusiana na kiwango cha uharibifu kwenye eneo lililoathiriwa.
j) Matumizi ya simu za satelaiti wakati wa dharura.

### 2.2.11 Matumizi ya Mawasiliano/ ya SimuTEHAMA na Tasnia ya Utangazaji katika Kuongeza Uelewa

Vyombo vya habari vina jukumu muhimu sana katika kuhabarisha na kutoa tahadhari ya kabla kwa umma, wakati na baada ya maafa, lakini katika kipindi cha miaka michache iliyopita, vyombo vya habari pia vimechukuliwa kama mpatanishi anayetoa elimu kuhusiana na maafa na hivyo kuufanya umma kuongeza jitihada za kufanya maandalizi ya maafa. Majukumu ya vyombo vya habari katika mazingira ya maafa yanaweza kudhihirika/kuonekana katika vipengele vifuatavyo.

a) Vyombo vya habari kutoa tahadhari za maafa na kuufahamisha umma kuhusiana na hali ilivyokuwa kabla, wakati na baada ya maafa kupitia televisheni, redio na mitandao ya kijamii,
b) Husambaza tahadhari za kabla na maelekezo/ushauri ili kuifanya jamii ijiandae kwa ajili ya maafa ya asili kama vile mafuriko, ambayo yako mbele yao,
c) Vyombo vya habari kama vile redio huwapa haki ya kupata taarifa waathirika na watu walioko kwenye mazingira hatarishi, ambao haki yao ya faragha inapaswa kuheshimiwa,
d) Vyombo vya habari huwapa haki ya kupata taarifa ambayo inapaswa kulindwa hata wakati wa dharura na maafa,
e) Vyombo vya habari hutoa taarifa za kuokoa maisha.

### 2.2.12 Ushirikiano na Wadau Mbalimbali (Sekta za Umma na Binafsi)

Utekelezaji wenye mafanikio wa NETP utahitaji ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na wadau mbalimbali. Aidha, utekelezahi huo utategemea dhamira ya dhati ya kila mdau, awe ni wizara za Serikali, wakala au sekta binafsi pamoja na Mawasiliano na ushirikiano madhubuti kati ya watoa huduma za Mawasiliano na serikali.

DMD kama wakala mkuu imeeleza majukumu ya kila mdau kama ilivyofafanuliwa katika SOP yake. Hata hivyo, Mawasiliano ya simu yatahitaji kuainishwa zaidi au kugawanywa zaidi ili wadau wengi ndani ya eneo hili watambue wajibu wao kuhusiana na udhibiti wa maafa.

DMD itakuwa chombo kikuu katika kueleza majukumu na taratibu za wadau wote katika ngazi mbalimbali watakaofanya kazi ya kukabiliana na maafa/dharura au mabalaa. Orodha ya Wadau wakuu wa Kitaifa wa Kudhibiti Maafa, majukumu na wajibu wao vimefafanuliwa katika Jedwali la 7.

### 2.2.13 Mafunzo kwa Vitendo

Mafunzo kwa vitendo ndiyo njia bora ya kuziandaa timu kukabiliana vyema na dharura au maafa. Mafunzo haya yatahitaji kuandaliwa ili kuwashirikisha wadau na kuwafanya wafanye kazi pamoja ili kusimamia utoaji wa huduma kwenye matukio yasiyotarajiwa. Sehemu za mafunzo, mazoezi, warsha na vitendo vitaongeza ujuzi wa kuandaa mipango, kuwafanya wanachama kuboresha utendajikazi wao na kuzitambua fursa za kuuboresha uwezo wao wa kukabiliana na matukio halisi kwa ajili ya mafunzo, warsha, na elimu zaidi.

Mafunzo ya kiutendaji ni zana madhubuti ya kuzisaidia taasisi na wakala wa serikali katika kujipangia mipango na kujijengea uwezo. Katika muktadha wa Mawasiliano ya simu ya dharura, mafunzo ya kiutendaji yanaweza kuanzishwa ili[9]:

a) Kuipima mikakati ya kitaifa na ile ya maeneo mahalia, itifaki na mifumo ya matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kukabiliana na maafa;
b) Kuongeza uelewa wa kanuni za Mawasiliano ya simu na jukumu lake muhimu katika kukabiliana na maafa;
c) Kutambua mapungufu na changamoto zinazoweza kutatuliwa kwa kufanya maandalizi katika sekta ya Mawasiliano ya simu ya dharura;
d) Kuongeza uelewa wa mbinu za kukabiliana;
e) Kutekeleza mipango ya dharura ya kitaifa/miongoni mwa wakala na/au mipango mahususi ya maeneo mahalia katika kufanya maandalizi ya kukabiliana na dharura;
f) Kujaribia sera, taratibu au vifaa vipya kabla ya kuingizwa katika mipango ya kitaifa;
g) Kutathmini majukumu na wajibu wa wadau wakuu katika kufanya maandalizi ya kukabiliana na dharura, ikiwa ni pamoja na jamii na serikali, mashirika ya forodha, sekta binafsi, wakala wa kitaifa wa kukabiliana na maafa, Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) za ndani na za kimataifa, ulinzi wa kiraia na mashirika ya Umoja wa Mataifa;

[9]ITU Emergency telecommunications table-top simulation guide

h) Kupima mbinu za kitaifa za uratibu wa kukabiliana na maafa na pamoja na uratibu wake kwenye makundi mengine katika ngazi ya mikoa;

i) Kuwasaidia wafanyakazi wa menejimenti ya kukabiliana na maafa katika majukumu na wajibu wao hususani katika matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya udhibiti wa maafa ya kitaifa na kiwilaya, kwa kuzingatia lengo mahususi kwenye awamu husika;

j) Kujenga uelewa wa miundo ya serikali na/au uratibu, ushirikiano na Mawasiliano kati ya Serikali na jumuiya/mashirika ya kibinadamu yaliyopo nchini;

k) Kushughulikia vihatarishi vinavyojitokeza katika sekta ya Mawasiliano ya simu ya dharura na kupima uratibu na upashanaji habari miongoni mwa sekta binafsi za TEHAMA;

l) Kubainisha kama mbinu, mifumo na rasilimali sahihi, ikiwa ni pamoja na mifumo ya kutoa tahadhari za kabla, inapatikana nchini na katika ngazi za kikanda na kimataifa, ili kusaidia matumizi ya TEHAMA na teknolojia katika majukwaa mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na dharura kwa mawanda mapana;

m) Kusaidia katika ujenzi wa uhusiano wa kisekta, ndani ya serikali na kati ya wadau wengine wakuu;

n). Kutumia mafunzo yaliyopatikana, kuunganisha mbinu bora zilizobainika wakati wa mafunzo kwa vitendo na kubainisha hatua zinazofuata ili kuimarisha maandalizi kwa ajili ya maafa yanayokuja.

### 2.2.14 Msaada kwa Watu Wenye Mahitaji Maalum

Utoaji wa elimu kwa watu wenye ulemavu, akina mama, watoto, wazee na wanawake kuhusiana na stadi za maisha, stadi za kujihifadhi/tunza, hadhari na hatua za kiulinzi na kiusalama, maandalizi ya msingi ya kukabiliana na maafa, mbinu za msaada wa kisaikolojia na hatua za kuzuia utapiamlo.

### 2.2.15 Taratibu Bora za Utendajikazi (SOP)

Taratibu Bora za Utendajikazi (SOP) ni miongozo au maelekezo rasmi yaliyoandaliwa kwa ajili ya kukabiliana na matukio, ambayo kwa kawaida huwa na vipengele vya uendeshaji na kiufundi na huwawezesha watoa huduma za dharura kufanya kazi katika muundo ulioratibiwa kwenye sekta/taaluma mbalimbali wakati dharura inapotokea.

SOP zitaelezea mfumo na michakato ya usambazaji wa taarifa wakati wa maafa na kwenye mazingira hatarishi. Usambazaji wa taarifa, kabla, wakati na baada ya maafa ni kipengele muhimu cha maandalizi ya kukabiliana na maafa.

SOP zitasimamia jinsi ya kusambaza taarifa endelevu kwa watu walioko kwenye maafa/vihatarishi na watu walioathiriwa kabla, wakati na baada ya maafa. Kila mdau anayejihusisha katika udhibiti wa maafa/dharura atalazimika kuandaa SOP zake za ndani.

SOP zimefafanuliwa kuwezesha utoaji wa Mawasiliano ya simu ili kusaidia udhibiti wa maafa. SOP zimefafanuliwa katika **Kiambatisho I**

### 2.2.16 Orodha ya Maofisa wa Mawasiliano

Orodha ya maofisa watakaohusika na huduma za Mawasiliano ya simu wakati wa maafa katika ngazi mbalimbali itaandaliwa katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya ikitoa majina yao, anwani, namba za simu, baruapepe n.k. Orodha hiyo itasambazwa kwa wingi na kuhuishwa kila mwaka. Orodha ya maofisa wa sasa iko kwenye **Kiambatisho II**.


## 2.3 Awamu ya Kukabiliana na Dharura na Maafa

Awamu hii itahitaji utekelezaji wa taratibu za uendeshaji/utendajikazi kama vile kutoa taarifa kwenye kurasa za wavuti/tovuti na maagizo ya kuondoka maeneo hatarishi, kusanidi viungo vya redio za muda, matengenezo ya intaneti za kitaifa na kimataifa na uamilishaji wa mifumo ya vitahadharishi vya dharura. Utoaji huduma za Mawasiliano ya simu ya dharura Kitaifa utahitaji kujizatiti kikamilifu kwa upande wa wadau wote wanaohusika. Hili litahitaji kuwa na mtazamo chanya kwenye mpango wa utoaji wa huduma. Mpango huo, utaamilishwa wakati wa maafa na utatumika kama njia ya Mawasiliano wakati wa dharura na maafa.

### 2.3.1 Tamko la Dharura

Ofisi ya Waziri Mkuu itatangaza dharura au maafa kwa umma na taasisi za serikali kupitia vyombo vya habari au majarida ya serikali, kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya 2023 (32). Aidha, uamilishaji wa Mpango wa Taifa wa Maandalizi na Utoaji wa Huduma za Dharura utaanza mara moja ili kuruhusu kila sekta kutoa huduma.

Kwa upande wa mchakato wa Mawasiliano ya simu, tamko hilo linaweza kutazamwa na kufuatwa kwa kutumia mtiririko wa chati ifuatayo iliyooneshwa kwenye Kielelezo 6 kwa hatua bora za Utoaji wa Huduma za Mawasiliano ya simu ya Dharura.




*Kielelezo cha 6: Taratibu za utoaji wa huduma za Mawasiliano ya simu za dharura*

Mfumo wa utoaji wa huduma za dharura utaanzishwa ili kuhakikisha kuwa, timu ya Mawasiliano ya Dharura inafanya kazi kwa ukaribu na Idara ya Kukabiliana na Dharura Kitaifa katika OWM - wanaotekeleza wajibu na majukumu yao maalumu. Ili kufikia hatua hii, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

i. Kukusanya rasilimali za ziada kutoka asasi zingine kadri inavyowezekana mf. kutoka redio za ridhaa, sekta binafsi na mashirika ya kimataifa.

ii. Kujibu maombi ya mashirika ya kitaifa na kimataifa ya misaada ya kibinadamu katika usambazaji wa vifaa vya Mawasiliano ya simu (kutoa

leseni kwa vifaa vinavyoingia nchini na kutoa masafa yaliyoombwa na mashirika hayo.

iii. Kutoa vifaa au huduma zinazofaa za Mawasiliano ya simu kwa maofisa wa Utafutaji na Uokoaji na kwa wale wanaotoa huduma kama vile matibabu, malazi, afua, usambazaji wa chakula, maji, n.k.

Mpango wa utoaji wa huduma za Mawasiliano ya simu ya Dharura umebainisha mambo yafuatayo katika utendajikazi wakati wa maafa au dharura:

i. Kuwezesha Mawasiliano ndani na nje ya nchi,
ii. Kuwezesha utoaji wa vifaa na/au huduma zinazofaa za Mawasiliano ya simu ili kuhakikisha kuna Mawasiliano ya simu yanayokidhi mahitaji ya dharura, hususani kwa watoa huduma za dharura na tasnia ya Mawasiliano ya simu.
iii. Kupokea na kuchambua maombi ya masafa ya ziada ya redio, kwa ajili ya matumizi ya vituo vya satelaiti au kutatua matatizo ibukizi ya mwilingiliano wa redio zaidi ya moja. Maombi ya dharura yaliyotolewa wakati wa dharura yatapaswa kushughulikiwa haraka iwezekanavyo.
iv. Wajibu wa kiufundi kwa ajili ya uundaji na uanzishaji wa mfumo wa utoaji tahadhari unaweza kutolewa kwa idara ya Mawasiliano ya dharura, lakini uamuzi wa kuanzisha na kusambaza ujumbe ni jukumu la watoa huduma.

Mpangilio wa kina wa wajibu kati ya wadau tofauti umeoneshwa kwenye Jedwali la 5

Jedwali la 5: Mpangilio wa uwajibikaji baada ya tamko la dharura

| Na. | Asasi | Wajibu na Majukumu |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Waziri Mkuu-Idara ya Menejimenti ya Maafa (DMD) | a) Kuanzisha mfumo wa Mawasiliano na taarifa za dharura;<br>b) Kuidhinisha, kwa kushirikiana na matangazo makubwa na vyombo vya habari vilivyochukuliwa;<br>c) Kuwataarifu wakala kuhusiana na tamko na uishaji wa dharura;<br>d) Kuratibu utoaji wa huduma;<br>e) Kutangaza kuwa dharura imeisha; |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) | a) Kuhakikisha watoa huduma za Mawasiliano wanashauriwa kuhusiana na tamko na kuisha kwa dharura na wanaendelea kutaarifiwa kuhusiana na dharura hiyo.<br>b) Kufanya ukaguzi wa miundombinu ya Mawasiliano ili kubaini mahitaji ya Mawasiliano na kuhakikisha kuwa waendeshaji wanasambaza vifaa/rasilimali za Mawasiliano pale zinapohitajika zaidi. Taarifa lazima zipatikane kutokana na uwezo uliopo wa Mawasiliano ya simu/TEHAMA ambao unaweza kupatikana kwa ajili ya kukabiliana na maafa ya dharura. Miundombinu iliyoharibiwa na tathmini ya huduma vitahitaji kujumuisha walao mambo yafuatayo;<br>i. Mifumo ya Simu za Mkononi na redio;<br>ii. Huduma za usafirishaji vifaa vya mawasilino ya dharura<br>iii. Hali ya mifumo /mfumo wa simu za mkononi kwa umma;<br>iv. Upatikanaji wa mtoa huduma za VSAT ndani ya nchi<br>v. Uwekwaji wa mapema wa Vifaa vya dharura vya MSS<br>vi. Huduma za intaneti |
| 3. | Jeshi la Polisi Tanzania (TPF) | a) Kuanzisha kiungo cha Mawasiliano endelevu na ofisa mwandamizi katika tukio/eneo la dharura;<br>b) Kutoa wafanyakazi wenye simu za upepo ili kusimamia/kuwezesha safari za magari ya dharura;<br>c) Linapaswa kuwatahadharisha watu walioko kwenye hatari ya dharura. |
| 4. | Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji (FRF) | a) Kuratibu shughuli za zimamoto<br>b) Kuanzisha kiungo cha Mawasiliano endelevu na ofisa mwandamizi katika eneo la dharura;<br>c) Kutoa taarifa na ushauri kuhusiana na masuala ya zimamoto na uokoaji<br>d) Kuwatahadharisha watu walioko kwenye hatari ya dharura. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na | Kutoa huduma za hali ya hewa, tabia ya nchi na tahadhari kwa ajili ya usalama wa maisha na mali za umma wote kwa ujumla na watumiaji wengine mbalimbali ikiwa ni pamoja na usafiri wa anga, kilimo na usalama wa chakula, vyanzo vya maji, udhibiti wa maafa, afya na tasnia ya ujenzi kupitia Mawasiliano ya simu na utangazaji wa vyombo vya habari. |
| 6. | Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) | Kusambaza tahadhari za masuala yanayohusiana na jiolojia kwa umma na mashirika mengine kupitia EOCC. |
| 7. | Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania na AZISE zingine | Utoaji wa huduma ya kwanza na uratibu hususani katika eneo lao la utaalamu |
| 8. | • Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na ile inayojihusisha na Kamati za Udhibiti wa Maafa (Kamati za Kata na Vijiji au Mtaa) na wadau wengine wanaohusika.<br>• Wizara yenye dhamana ya Afya,<br>• Wizara yenye dhamana ya Mifugo,<br>• Wizara yenye dhamana ya Kilimo,<br>• Wizara yenye dhamana ya maji,<br>• Wizara yenye dhamana ya Maji, Sekretarieti za Mikoa (RS), Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) na wadau | a) Kupokea taarifa za tahadhari za maafa/dharura.<br>b) Kuwatahadharisha maofisa maalumu wa eneo husika kuhusiana na mazingira ya maafa.<br>c) Kusambaza taarifa za tahadhari na maelekezo kwa umma kupitia mifumo iliyopo ya tahadhari.<br>d) Kusambaza tahadhari na maelekezo kwa vituo maalum kama vile shule, magereza, nyumba za wazee, vituo vya kulelea watoto na hospitali. |

| | | |
|---|---|---|
| | wengine wanaohusika | |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD), Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania (TGFA). | a) Kutambua njia za usafirishaji za umma na za binafsi na kuratibu matumizi yake wakati wa dharura, hususani katika kutoa usafiri kwa ajili ya uhamishaji wa watu na mali zao.<br>b) Kuratibu usambazaji wa vifaa vya usafirishaji ili visaidie shughuli za dharura.<br>c) Kuanzisha na kuendeleza hifadhidata ya madereva, mafundi wa magari, vipuri na zana za magari.<br>d) Kuzisaidia serikali za mitaa katika kutathmini njia nzuri za usafiri zaidi katika maeneo yaliyoathiriwa na kuanzisha njia mbadala za usafirishaji wa watu, bidhaa na huduma. |
| 10. | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), RS, LGAs, TRCS, Jeshi la Polisi Tanzania, Chama cha Skauti Tanzania, Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kimataifa/Kikanda, Kampuni ya Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), AZISE, Kampuni Binafsi, Vitengo vya Usimamizi wa Fukwe na Watu Wenye Ujuzi, TPDF pamoja na wadau wengine wanaohusika. | a) Kuratibu na kuendesha shughuli za utafutaji na uokoaji.<br>b) Kutambua mahitaji ya rasilimali maalum ili kusaidia shughuli za uokoaji.<br>c) Kuratibu msaada wa nje wa kiufundi na vifaa.<br>d) Kusaidia kwa ajili ya shughuli za utafutaji na uokoaji. |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Watoa Huduma - (Waendeshaji wa Mitandao wa Simu, TV, Redio) | a) Kuwezesha tahadhari na kuhuisha taarifa zilizotolewa vibali kutoka kwenye OWM – DMD kwa ajili ya maafa.<br>b) Kuhakikisha mwendelezo wa Mawasiliano hususani, kwenye maeneo yaliyoathirika.<br>c) Kushughulikia vipengele vyovyote vya kiutekelezaji ambavyo vitawezesha Kukabiliana na Dharura.<br>d) Kutunza kumbukumbu na logi za redio za hatua zote kwa ajili ya kupata na kutoa taarifa baada ya dharura ambayo itakuwa imeandaliwa. |

### 2.3.2 Ukusanyaji na Uchambuzi wa data/taarifa kuhusiana na mahitaji ya haraka

Data/taarifa wakati wa kukabiliana na maafa ni lazima zikusanywe vizuri na ni lazima ziwe sahihi, ili kuhakikisha taarifa muhimu zinatolewa kwa umma na/au kwa wafanyakazi wa kutoa misaada, kwa kuzingatia madhara yaliyosababishwa na maafa, mfano wa taarifa inayohitajika ni uelekeo wa eneo ambapo timu za uokoaji zitapelekwa na maeneo yaliyoathiriwa sana. Endapo kutakuwa na maafa, ruhusa ya kusambaza taarifa za kina za simu (CDR) kwa ajili ya taarifa za maelezo ya eneo husika, itachukuliwa kama ni jambo linaloruhusiwa kiotomati kwa muda wa zaidi ya wiki mbili.

Watoa Huduma za Mawasiliano watawasilisha Ripoti ya awali kwa TCRA kwa mujibu wa **Kiambatisho III** kuhusiana na mtandao wao na namba za dharura na kuzihuisha pindi inapohitajika.

### 2.3.3 Uelewa wa Kimazingira na Uhuishaji wa Taarifa

Timu ya kukabiliana na maafa na umma watapaswa kufahamishwa kuhusiana na hali ya eneo lililoathiriwa na maafa kwa kutumia data ya picha za kamera zisizokuwa na rubani (droni) pamoja na vituo vingine vya kukabiliana na maafa.

### 2.3.4 Kuunganisha familia na marafiki

Watu walioathiriwa watakuwa na uwezo wa kuwataarifu wengine kuhusiana na hali zao na mahali walipo kwa kuwasiliana na ndugu/wapendwa wao kwa arafa wakitumia namba za utambulisho wa vifaa (IP) vinavyotumia mtandao na mifumo mingine ya utoaji taarifa za maafa. Hata hivyo, watoa huduma watapaswa kuhakikisha kuwa, hakuna mteja atakayeshindwa kupata Mawasiliano ya sauti/ARAFA kwa sababu zozote za kibiashara ikiwa ni pamoja na kutolipa/kutokuwa na salio la kutosha/kutozwa tena n.k. Kituo hiki kitaendelea kwa angalau siku 15.

### 2.3.5 Ukusanyaji Pamoja wa Vifaa

Watoa huduma za Mawasiliano watatumia vifaa/rasilimali kwa pamoja ikiwa ni pamoja na kutumia simu ya mtandao mwingine kitaifa (Mkataba wa Makubaliano utatakiwa kuwapo) ili huduma zitolewe kwa umma na kwa makundi ya watumiaji waliopewa kipaumbele bila masharti.

## 2.4 Afua Zinazotolewa Wakati wa Udhibiti wa Dharura na Maafa

Awamu ya urejeshaji itajikita katika kutoa msaada unaohitajika ili jamii irejee katika hali yake ya kiusalama na kiutendajikazi kabla ya dharura. Katika awamu hii, wadau watafanya kazi ya kurejesha miundombinu iliyoharibiwa ya Mawasiliano ya simu/TEHAMA, kujenga upya na kuboresha miundombinu ya mitandao ya Mawasiliano ya simu/TEHAMA na itahusisha usambazaji wa mitandao kwa ajili ya kujiandaa kwa maafa yajayo. Mitandao na huduma za Mawasiliano ya simu/TEHAMA vitatumika kusaidia tathmini ya uharibifu na hasara, mahitaji ya maeneo na watu walioathirika, kubainisha maeneo yenye mahitaji ya msaada wa urejeshaji wa hali, kufuatilia shughuli za urejeshaji na kuratibu shughuli za ujenzi mpya.

### 2.4.1 Tathmini ya Taarifa za Uharibifu na Mahitaji

Sehemu hii itatoa tathmini sahihi ya athari za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja za tukio la dharura na maafa na madhara yake kwa ustawi wa kijamii na shughuli za kiuchumi kwa jamii au watu walioathirika. Tathmini itajikita kwenye taarifa zilizokusanywa kuhusiana na uharibifu kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya taarifa za kianolojia na kidijitali kama vile hojaji za utafiti, makala za wanahabari pamoja na mahojiano na jamii iliyoathirika. Zana za Mawasiliano ya simu/TEHAMA zitahitajika kwa haraka ili kutathmini na kutaratibu kiwango cha uharibifu na hasara, kusaidia kutoa maelezo ya mikakati ya ujenzi upya, kuweka misingi ya masharti ya kijiografia na kisekta na kusaidia kutoa ufafanuzi wa vipaumbele. Hili litahusisha:-

a) Kuyatambua na kuyawasilisha maeneo yanayohitaji urejeshaji kwenye vikundi vinavyotoa msaada huo;
b) Kutoa mwongozo wa kutambua hatari na/au mifumo mipya ya alama za mpito iliyoko kwenye mazingira magumu;
c) Kutathmini ufaafu wa mipango ya uendelezaji upya;
d) Kuzitambua hatua faafu za kukabiliana na tukio la maafa ya siku zijazo;
e) Kuyatambua mabadiliko yanayohitajika katika shughuli za maandalizi na makabiliano dhidi ya maafa/dharura zijazo;
f) Kutoa mwongozo wa kuzibainisha athari za maafa za muda mrefu kama vile mafuriko makubwa;
g) Kutoa mwongozo utakaotumika kufuatilia maendeleo ya shughuli za urejeshaji upya wa hali.

### 2.4.2 Kujenga Upya na Kuboresha Miundombinu ya Mawasiliano/TEHAMA

a) Kurejesha upya Miundombinu ya Mawasiliano/TEHAMA iliyoharibika;
b) Kuwa na matumizi ya muda ya huduma za simu kama vile matumizi ya simu za satelaiti;
c) Kuhakikisha kuwa usambazaji wa nishati ya umeme unakuwapo.

### 2.4.3 Kuunganisha Njia Mbadala na za Ziada katika Mitandao ya Mawasiliano/TEHAMA

Mitandao ya Mawasiliano ya simu/TEHAMA kama vile vituo vya simu za mkononi, swichi za ndani na nyaya za usambazaji/upitishaji kama vile Waya wa Kupitisha Picha vinaweza kuharibika sana wakati wa maafa au hali za dharura kama vile maafa makubwa ya asili. Ili kukabiliana vyema na dharura hizi za baada ya maafa, ni muhimu kuunganisha pamoja njia mbadala na za ziada za Mawasiliano/TEHAMA ili kupunguza changamoto za Mawasiliano, kuwezesha ukusanyaji wa taarifa na kutoa njia za Mawasiliano kwa kutumia kila mbinu inayowezekana hasa wakati wa dharura. Ili kukabiliana na changamoto hii, teknolojia na hatua zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa.

a) Matumizi ya Mawasiliano ya Satelaiti

Matumizi ya vituo rahisi vya ardhini vinavyowezesha Mawasiliano ya satelaiti na simu za mkononi yatapaswa kuruhusiwa katika hali za dharura au maafa.

b) Katika Mitandao ya Pamoja/Upatikanaji wa Mitandao. Lengo hili linaweza kufikiwa kwa:

i. Matumizi ya Vipuri kwa ajili ya kubadilishia vifaaswichi na vifaa vya kupitisha/kusambaza Mawasiliano.
ii. Kuwa na njia nyingi za vifaa vya kupitishia/kusambazia Mawasiliano.
iii. Kuweka kifaa cha kiotomati cha kugundua msongamano, kusimamia na kudhibiti usafirishaji
iv. Kuweka vitahadharishi vya kiotomati vya moto na mifumo ya zimamoto
v. Kuhifadhi vifaa kwenye mazingira mazuri ili visiharibike
vi. Kuwa na vifaa vizuri vya nje na majengo imara ili kupunguza athari za maafa
vii. Kuongezeka uwezo wa njia mbadala
viii. Kuweka kipaumbele kwenye simu za dharura kwa ajili ya kudhibiti Msongamano.

c) Katika upatikanaji wa Mtandao muda wote na Kituo cha Mawasiliano

- Simu maalum za bila malipo kwa umma
- Simu za mkononi za satelaiti

d) Katika upatikanaji wa Simu za Mkononi na Kituo cha Mawasiliano
    - Punguza ubora wa Mawasiliano ya simu sauti ili kudhibiti Msongamano

e) Kwa ajili ya Upatikanaji wa Intaneti
    - Kutoa huduma za Intaneti bila malipo kwa njia isiyo na waya (wireless) na ikiwa ni pamoja na vituo vya uhamishaji/uokoaji
    - Kuweka kipaumbele cha usafirishaji kwa ajili ya usimamizi wa upokeaji na utumaji wa taarifa (usimamizi wa kipimodata)

f) Kwa usambazaji wa Nishati ya Umeme
    - Matumizi ya vifaa rahisi vya kusambazia nishati ya umeme na jenereta au betri za umeme.

**2.4.4 Kutambua maeneo yanayohitaji msaada wa urejeshaji na shughuli za ufuatiliaji wa afua**

Kuhakikisha kuna uratibu kwa watoa huduma za miundombinu ya Mawasiliano ya simu ili kufikia azima ya pamoja.

**2.4.5 Kuratibu Shughuli za Ujenzi Upya**

Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa serikali kuhusiana na miundombinu ya Mawasiliano ya simu na miradi mingine inayohusiana wakati wa awamu ya ujenzi.

## 3. MPANGO WA UTEKELEZAJI NA VIPIMO

Utekelezaji mzuri wa mpango huu utatokana na bidii za wadau mbalimbali wanaohusika katika mpango huo. Mawasiliano ya simu/TEHAMA kwa ajili ya Menejimenti ya Maafa yanaweza kujumuishwa kwa muhtasari katika kanuni nne: taarifa za majanga mbalimbali, taarifa za matumizi ya teknolojia mbalimbali, taarifa za Utekelezaji wa awamu mbalimbali, na taarifa za Ushirikiano wa wadau mbalimbali. Jedwali la 6 linaonesha majukumu na wajibu kwa ajili ya utekelezaji wa Mawasiliano ya Dharura.

### 3.1 Taarifa za Majanga Mbalimbali

Majanga yanajumuisha yale ya asili na yale yanayotokana na shughuli za kiteknolojia za binadamu. Majanga ya asili ni pamoja na matetemeko ya ardhi, vimbunga, mafuriko,

umeme, maporomoko ya matope/maporomoko ya ardhi, ukame, tsunami, milipuko ya volkeno, moto na magonjwa tandavu. Majanga yanayotokana na shughuli za kiteknolojia za binadamu ni pamoja na milipuko ya moto, kuporomoka kwa majengo, machafuko ya kiraia, dharura mseto, ajali za malori kumwaga mafuta, ugaidi, Ajali na Milipuko ya Viwandani. Kwa maafa yote yanayotokana na majanga ya asili na yanayotokana na shughuli za kiteknolojia za binadamu, TEHAMA huwa na jukumu muhimu katika kuwezesha mara moja mtiririko wa taarifa muhimu.

### 3.2 Taarifa za Matumizi ya Teknolojia Mbalimbali

Katika kupunguza athari za maafa yanayotokana na majanga, inashauriwa kuwa Serikali itahamasisha matumizi ya teknolojia mbalimbali za habari na Mawasiliano na mitandao ikiwa ni pamoja na satelaiti, Redio ya Masafa Marefu (HF Radio) na Redio za Masafa Mafupi na ya Kati (VHF Radio), redio za utangazaji, televisheni, mitandao ya simu isiyohamishika na isiyotumia waya na mitandao mingine kama vile, mitandao ya kijamii, televisheni mtandao na magazeti ya mtandaoni, blogu na tovuti ambazo zinaweza kuchangia kuongeza uwezo na kupunguza uwezekano wa watu kuathirika.

### 3.3 Taarifa za Ushirikiano wa Wadau Mbalimbali

Utekelezaji mzuri wa NETP unategemea zaidi uratibu na ushirikiano mkubwa kati ya wizara zote, taasisi, idara, jamii mahalia (eneo hilo), sekta binafsi, Mashirika ya Misaada ya Kibinadamu, mashirika ya kimataifa na Jamii zilizopewa wajibu wa kutoa huduma nyakati za maafa au dharura. Wakati wote uratibu utahusisha DMD - OWM, mamlaka, waendeshaji na mashirika mengine yenye wajibu huo iwe kwa kupitia serikali au njia nyingine katika kuisaidia serikali ya Tanzania wakati wa maafa au dharura. Kwa hiyo, huduma bora ya TEHAMA/Mawasiliano ya simu zitahitajika kuwapo ili kuhakikisha uratibu unafikiwa wakati wa maafa au dharura.

### 3.4 Taarifa za Utekelezaji wa Awamu Mbalimbali

Mawasiliano ya simu ni muhimu katika hatua zote za kudhibiti maafa: kupunguza, kufanya maandalizi, kutoa huduma na misaada, kurejesha na kukarabati.

Jedwali la 6: Majukumu na wajibu kwa ajili ya kukabiliana na Dharura

| Na. | Asasi | Wajibu na Majukumu |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Menejimenti ya Maafa (DMD) | a) Kitengo kikuu cha Kitaifa cha uratibu na Mawasiliano kwa ajili ya udhibiti wote wa maafa na upunguzaji wa vihatarishi.<br>b) Kuhakikisha utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano ya Maafa |

| | | |
|---|---|---|
| | | c) Kujumuisha vifaa zaidi vya Mawasiliano ya simu kwenye Kituo cha Uendeshaji na Mawasiliano ya Dharura (EOCC) ili vitumike katika awamu zote za udhibiti wa maafa ikiwa ni pamoja na utoaji wa tahadhari za mwanzo. Kuorodhesha vifaa vya TEHAMA na simu za mkononi.<br>d) Kujumuisha wadau zaidi kwenye EOCC, ili kuratibu shughuli za maandalizi na utoaji wa huduma katika ngazi ya kitaifa, ikizihusisha taasisi/mashirika ya umma na binafsi.<br>e) Kuhakikisha kuwa vifaa vyote vilivyonunuliwa vinakidhi mahitaji ya PPDR.<br>f) Kutengeneza zana za usimamizi kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa wadau katika kujiandaa kukabiliana na maafa. |
| 2. | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | a) Kutoa maelekezo ya jumla ya Kisera kuhusiana na matumizi ya Mawasiliano/TEHAMA katika kudhibiti maafa<br>b) Kuidhinisha Mkataba wa Tampere unaohusu Utoaji wa Vifaa vya Mawasiliano kwa ajili ya Kupunguza athari za Maafa na Utoaji wa Misaada.<br>c) Kuufanya Mkataba wa Tampere na masharti yake viendane na sheria na kanuni za Kitaifa za Mawasiliano/TEHAMA. |
| 3. | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) | a) Kuandaa na Kutekeleza NETP katika ngazi ya kitaifa ikihusisha wadau wote wakuu katika ngazi ya kitaifa na kijamii.<br>b) Kubainisha majukumu kwa viongozi wanaotumia TEHAMA kwa ajili ya udhibiti wa vihatarishi vya maafa katika ngazi ya kitaifa ili kuhakikisha hatua zinachukuliwa na kwamba kuna uwajibikaji na uendelezaji wa majukumu.<br>c) Kuhakikisha kuna njia nyingi za kuunganisha (na za ziada) kwenye EOCC ili kuzifungamanisha pamoja teknolojia mbalimbali.<br>d) Kuandaa na kupitisha mfumo wa usimamizi/udhibiti kwa madhumuni ya Mawasiliano ya dharura<br>e) Kuyajumuisha masharti katika mfumo wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | usimamizi/udhibiti wa sekta binafsi ili kuiwezesha miundombinu ya Mawasiliano na huduma zake katika awamu zote za udhibiti wa maafa kusambaza taarifa muhimu na kwa wakati pindi zinapohitajika.<br>f) Kuuandaa, kupitisha na kuufanyia mapitio ya mara kwa mara mpango wa Mawasiliano ya dharura. |
| 4. | Wizara zenye dhamana ya Habari, Afya, Kilimo, Mifugo, Maji, Mamlaka ya Hali ya Hewa, Utafiti wa Kijiolojia Tanzania, Kamati za Udhibiti wa Maafa na Sekta Binafsi | a) Kuimarisha mifumo ya Mawasiliano ya redio kwa matumizi ya ndani;<br>b) Kuwezesha upatikanaji wa mifumo ya Mawasiliano kwa ajili ya Mawasiliano ya dharura;<br>c) Kuimarisha orodha ya vipuri vya mifumo ya redio;<br>d) Kufanya mazoezi na majaribio ya uwezo wa Mawasiliano ya redio;<br>e) Kuipatia taarifa za mara kwa mara OWM;<br>f) Kuimarisha mikataba/makubaliano na watoa huduma za Mawasiliano kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya vifaa vya Mawasiliano;<br>g) Kuimarisha mitandao ya nchi nzima na mifumo ya misaada ya pande zote pindi inapohitajika;<br>h) Kutoa njia zinazoingiliana za masafa ya Mawasiliano kwenye EOC kwa matumizi ya uratibu wa misaada ya pande zote au uendeshaji/shughuli za pamoja na mashirika mengine;<br>i) Kubainisha athari za dharura kwenye mifumo ya Mawasiliano na kuanzisha shughuli za ukarabati;<br>j) Kuitumia mifumo ya Mawasiliano kupitishia taarifa muhimu kutoka kwa vitengo vya ugani/maeneo husika hadi kwenye EOC;<br>k) Kuiruhusu OWM na mashirika mengine kadri itakavyowezekana kutumia mifumo ya Mawasiliano, vifaa na wafanyakazi ili kuwasilisha taarifa za dharura;<br>l) Kutekeleza sera zinazohusiana na matumizi ya mifumo inayoingiliana ya Mawasiliano kwenye maafa. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Jeshi la Polisi Tanzania (TPF); | a) Kulinda amani, kusimamia sheria na taratibu, kuzuia na kubaini uhalifu, kuwakamata na kuwalinda wakosaji pamoja na kuwalinda watu na mali zao. |
| 6. | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF) | a) Kuzuia na kupunguza idadi ya vifo, madhara kwa watu na uharibifu wa mali unaotokana na moto, mafuriko, matetemeko ya ardhi, ajali za barabarani na maafa mengine. |
| 7. | Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) | a) Kuzisaidia Mamlaka za kiraia pale ambapo msaada huo unahitajika ili kuzuia vifo au upotevu wa mali |
| 8. | Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) | a) Kufanya utafiti na kutoa mafunzo ya hali ya hewa na hali ya tabia ya nchi pamoja na nyanja zingine zinazohusika na kushirikiana na taasisi zingine pale inapolazimu kwa ajili ya matumizi ya mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.<br>b) Kutoa huduma za hali ya hewa na tabia ya nchi pamoja na tahadhari kwa ajili ya usalama wa maisha na mali kwa umma wote na watumiaji wengine ikiwa ni pamoja na usafiri wa anga, kilimo na usalama wa chakula, vyanzo vya maji, menejimenti ya maafa, afya na sekta ya ujenzi; |
| 9. | Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) | a) Ufuatiliaji wa Matetemeko ya Ardhi na Milipuko ya Volkano<br>b) Kusambaza tahadhari zinazohusiana na taarifa za maafa ya kijiolojia kwa umma kupitia EOCC |
| 10. | OR-TAMISEMI | a) Kuhakikisha uanzishwaji wa EOCC katika kila ngazi ya mtaa<br>b) Kutoa mafunzo na uelewa kwa jamii mahalia. |
| 11. | Mamlaka ya Serikali Mtandao (EGA) | a) Hakikisha kuwa Wizara, Idara na Mashirika yote ya Serikali na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zimeunganishwa kwenye EOCC<br>b) Kuhakikisha kuwa mifumo yote ya taarifa za Wizara, Idara na Mashirika ya Serikali pamoja na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zinafuata Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019. (E-Gov. Act 2019). |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Wizara ya Afya | a) Kuwasilisha Taarifa zote za maafa yanayohusiana na afya kwa EOCC<br>b) Kutoa mafunzo na uelewa wa masuala ya maafa yanayohusiana na afya kwa umma wote |
| 13. | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) | a) Kufanya usimamizi wa ulinzi na usalama wa sekta ya anga<br>b) Kunganisha na Kuwasilisha masuala yote ya maafa yanayohusiana na Taarifa za usafiri wa anga kwa EOCC<br>c) Kutoa mafunzo na uelewa wa masuala ya maafa kwa Mashirika yake (Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania - TAA, Mashirika ya Ndege, Kampuni)<br>d) Kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji wa ndege |
| 14. | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC) | a) Kuunganisha na Kuwasilisha Taarifa zote zinazohusiana na maafa ya kimazingira na kemikali kwa EOCC<br>b) Kufanya ukaguzi na kuhakikisha kuwa hatua za kurekebisha zinachukuliwa ikiwa hali hatarishi au hali mbaya zitabainika. |
| 15. | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) | a) Kuunganisha na Kuwasilisha Taarifa zote za maafa ya baharini kwa EOCC<br>b) Kuratibu masuala yote yanayohusiana na shughuli za kitaifa za utafutaji na uokoaji baharini<br>c) Kusambaza taarifa na kujenga uelewa wa masuala yanayohusiana na mazingira, ulinzi na usalama wa baharini. |
| 16. | Wizara, Idara na Mashirika Mengine ya Serikali | a) Kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kitaifa kuhusiana na udhibiti wa maafa<br>b) Kushirikiana vyema na wadau wengine katika masuala ya udhibiti wa maafa. |

| | | |
|---|---|---|
| 17. | Watoa Huduma - (Waendeshaji wa Mitandao ya Simu za Mkononi, Wato Huduma za Intaneti (ISP), TV, Redio) | a) Kuhakikisha uimara/uthabiti wa mitandao ya Mawasiliano kwa kushirikiana na wadau wengine kwa kuwa na mipango ya dharura mfano miundombinu inayohamishika kama vile Vifaa vya Kusambaza na Kupokea Mawasiliano (BTSs).<br>b) Kutoa taarifa kwa umma kwa wakati pindi maafa yanapotokea. Hawa wanaweza kutumika kutoa taarifa kwa wakati kwa umma na kuhakikisha kuna Mawasiliano katika ngazi zote za serikali pindi maafa yanapotokea.<br>c) Kuanzisha kanzidata nzuri ili kuunga mkono awamu zote za mfuatano wa udhibiti wa maafa, kwa kuzingatia viwango vilivyotengwa kama vile vinavyohusiana na usalama wa taifa, utunzaji wa data na faragha kama ilivyoelezwa na kufikiwa kwa kutumia matangazo ya simu, uwekaji wa uzio ramani (*geo-fencing*) na kutumia uwezo wa CAP.<br>d) Kusaidia katika awamu zote za udhibiti wa maafa kadri inavyowezekana kwa kupitia uwezo, nafasi, rasilimali na mamlaka yao mf. kuweka simu za kipaumbele wakati wa maafa.<br>e) Kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu ili kunufaika na matumizi sahihi ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na Mawasiliano ya zamani na mapya, katika kuokoa maisha ya watu na njia zao za uzalishaji mali.<br>f) Kuhakikisha kuna ulinganifu/ufanano ili kuwezesha utangamano/mwingiliano miongoni mwa watoa huduma za Mawasiliano wakati na baada ya maafa.<br>g) Kila MNO atapaswa kuupitia upya, kuuhuisha na kuutekeleza Mchakato wake wa Majaribio ya Urejeshaji wa hali baada ya Maafa wakati wowote ambapo kuna mabadiliko katika topolojia ya mtandao ili kuimarisha maandalizi. |
| 18. | Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania na AZISE zingine | Kupanga na kutoa mafunzo ya huduma ya kwanza pamoja na uratibu hususani katika eneo la utaalamu wao |

| | | |
|---|---|---|
| 19. | Mashirika ya Kimataifa na Vyombo vya Kikanda - Chama cha Mawasiliano ya Kimataifa (ITU) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) | Kutoa msaada katika Kuuendeleza NETP kwa kubainisha:<br>a) Miongozo kwa ajili ya wadau kufanya kazi pamoja na kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia zilizopo na zinazoibukia za Mawasiliano/TEHAMA ili kuokoa maisha ya watu, kazi pamoja na mali zao.<br>b) Mafunzo kwa vitendo/mazoezi ya mara kwa mara ili kupima utayari wa mfumo na watu<br>c) Taratibu za kawaida za utendajikazi kwa ajili ya uandaaji na usambazaji wa taarifa za tahadhari za mwanzo kwa kutumia njia zote za TEHAMA<br>d) Masharti mahususi kwa ajili ya jamii ya Watu Wenye Ulemavu |

### 3.5 Mapitio ya Mpango

Kwa kuzingatia kwamba teknolojia ya Mawasiliano inabadilika kwa kasi, NETP utapitiwa mara kwa mara na kwa angalau kila baada ya miaka mitatu. Mapitio hayo yatazingatia matokeo ya mafunzo kwa vitendo na maafa halisi. Zaidi ya hayo, mapitio ya **Kiambatisho II** yatafanywa kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 2.2.16.

## 4. HITIMISHO

Mpango huu wa Taifa wa Mawasiliano ya Dharura ni sehemu muhimu ya Mpango wa Taifa wa Kusimamia Maafa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Namba 6 ya 2022. Malengo ya muda mrefu na malengo ya muda mfupi ya NETP hayawezi kufikiwa bila msaada na uratibu wa wadau na timu ya kukabiliana na maafa. NETP utawasaidia wadau kuwa na mkakati wa pamoja wa kukabiliana na changamoto zinazotokana na maafa na majanga/matukio ya asili. Hatua zilizopendekezwa katika mpango huu zitasaidia kufikia maono ya pamoja na kutatua changamoto zilizotajwa katika Sera ya TEHAMA ya 2016, kupitia juhudi za pamoja za kuwawezesha watoa huduma za dharura kuwasiliana kama inavyotakiwa kabla, wakati na baada ya maafa au dharura.

## KIAMBATISHO I: SOP KWA AJILI YA MAWASILIANO YA DHARURA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Malengo

- Uratibu wa hatua za kitaifa ili kuhakikisha kuna utoaji wa msaada wa Mawasiliano ya simu katika ngazi za mamlaka ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya.
- Uratibu wa mahitaji ya huduma za Mawasiliano ya muda katika maeneo yaliyoathirika.
- Uratibu wa kurejesha huduma za Mawasiliano ya simu.

### 1.2 Vyombo/Asasi Muhimu

Ili kutoa huduma bora za Mawasiliano ya dharura na kurejesha huduma za kawaida za Mawasiliano, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (MICIT) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zitahitaji msaada kutoka kwa Wizara/Idara/Mashirika yafuatayo:

a) Watoa huduma za Mawasiliano
b) Watangazaji (wa Redio na Televisheni)
c) Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)
d) Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Menejimenti ya Maafa (OWM- DMD)
e) Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania
f) Jeshi la Polisi Tanzania
g) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania
h) Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD)
i) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF)
j) Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)
k) Wizara ya Afya
l) Wizara ya Kilimo
m) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)
n) Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania
o) Shirika la Reli Tanzania (TRC)
p) Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA)
q) Huduma za Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu
r) Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA)
s) Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)

## 2.0 MCHAKATO WA UTOAJI TAHADHARI KWA UMMA

Kama tahadhari kwa umma itathibitishwa na Idara ya Menejimenti ya Maafa (DMD), mchakato utakuwa ni kuwasiliana mara moja na 'kituo (kikuu) cha Mawasiliano ya kila kituo cha utangazaji cha redio, televisheni, vyombo vya habari vya mtandaoni na Waendeshaji wa Mitandao ya Simu za Mkononi (MNOs) kwa sharti la kuutangaza mara moja Ujumbe wa Tahadhari iliyoripotiwa awali. Ujumbe wa tahadhari utahitaji kutengenezwa ili kuendana na teknolojia mahususi na huduma mbalimbali zilizopo.

### 2.1 Utumaji wa Arafa

Kufuatia tahadhari rasmi ya maafa, mfumo wa utumaji wa arafa unaweza kutumika kusambaza taarifa kwa umma. Msimamizi wa EOCC ataandaa ujumbe (usiozidi herufi 90) ukilenga taarifa iliyotolewa. Ujumbe unaweza kutumwa kwa watumiaji wa simu walioko katika eneo lililowekwa uzio wa kijiografia (uzio ramani). Utumaji wa arafa unapaswa kuwasilishwa kwa MNO kwa ajili ya usambazaji kwenye simu za mikononi zinazotumika katika eneo lililowekwa uzio wa kijiografia.

### 2.2 Matangazo ya Redio na Televisheni

Redio na Televisheni ni nyenzo muhimu katika usambazaji wa taarifa. Iwapo kutakuwa na matangazo rasmi ya maafa, watangazaji wa redio na televisheni watatakiwa kusitisha programu zao za kawaida ili kutangaza tahadhari za dharura zilizoripotiwa awali ili kuwajulisha wasikilizaji na watazamaji wao kwamba kuna dharura inayotokea katika eneo lao. Zaidi ya hayo, watangazaji wa redio na televisheni watatangaza taarifa za majanga yaliyopo kutokana na taarifa zilizotolewa na taasisi zingine kama vile Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

### 2.3 Tovuti ya Idara ya Menejimenti ya Maafa (DMD)

Tovuti ya OWM ni wenzo muhimu wa Mawasiliano kwa umma na wadau. Maudhui ya tovuti hii lazima yahuishwe mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa wananchi na washirika wa DMD wanapewa taarifa zilizoidhinishwa rasmi. Tovuti ya OWM ina anwani ya: www.pmo.go.tz

### 2.4 Chaneli za Mitandao ya Kijamii (Facebook, Twitter, Instagram, Youtube na Blogu)

Kuwapo kwa OWM kwenye mitandao ya kijamii ni chaneli nyingine itakayomwezesha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (HGCU) kuwasiliana na wananchi ndani na nje ya eneo lililoathiriwa. Mitandao ya kijamii ni vyanzo muhimu vya taarifa kwa umma.

Ukurasa wa Facebook wa OWM, akaunti ya Twitter, akaunti ya Instagram, Youtube na blogu zinasimamiwa na HGCU. Ofisa Habari (IO) ana wajibu wa kuhakikisha kuwa vitu visivyohitajika vimeondolewa kabla ya kuchapishwa kwenye kurasa za OWM kwenye mitandao ya kijamii. IO atakuwa na jukumu la kuziondoa taarifa hizo pindi mtu anapoondoka au anapokuwa hazihitaji tena kama sehemu ya kazi zake.

**Facebook**

Ukurasa wa Facebook wa OWM kimsingi ni njia ya matangazo ya moja kwa moja kutoka kwa DMD hadi kwa umma, ingawa maoni yanaweza kutumwa na umma kwenye ukurasa wa Facebook wa OWM. Ukurasa utasimamiwa na HGCU. Akaunti ya OWM kwenye Facebook ni: OWM Sera Bunge Uratibu

**Twitter**

Ukurasa wa Twitter ya OWM ni: Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu @OWM_SBU na inasimamiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

**Akaunti ya Instagram**

Akaunti ya Instagram ya OWM ni; ofisi_ya _ waziri_mkuu_sbu. Akaunti hiyo inasimamiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

**Akaunti ya YouTube**

Akaunti ya YouTube ya OWM ni; URATIBU_ONLINE_TIVE. Akaunti inasimamiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

**Blogu**

Blogu ya OWM ni; wazirimkuu.blogspot.com. Ukurasa huo unasimamiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (HGCU).

## 3.0 MAWASILIANO YA REDIO (Masafa Marefu, Masafa Mafupi na ya Kati)

### 3.1 Redio ya Masafa Marefu na za Masafa Mafupi na ya Kati

Redio ya njia mbili humwezesha mwendeshaji/opereta kufanya mazungumzo na redio za njia mbili zinazofanya kazi kwa masafa ya redio sawa (chaneli). Tofauti na mifumo mingine ya Mawasiliano (kama vile simu ya mkononi), ujumbe kupitia mfumo wa redio za Masafa Marefu (HF) na za Masafa Mafupi na ya Kati (VHF) si wa faragha na unaweza kusikilizwa na watu wengine wanaosikiliza chaneli hiyohiyo ya redio. Ujumbe kutoka kwa redio ya HF na VHF utapaswa kuwa mfupi na wa uhakika ili chaneli isiparanganyike.

Miundombinu na Vifaa Vilivyopo chini ya Uangalizi wa DMD;

| Na. | Vifaa/Miundombinu | Mahali | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kituo tuli cha msingi cha redio ya HF isiyotumia waya | | |
| 2. | Kituo tuli cha msingi cha redio ya VHF | | |
| 3. | Redio ya gari ya VHF | | |
| 4. | Redio ya VHF ya vyombo vya uokoaji wa majini | | |
| 5. | Redio za VHF za vifaa vya uokoaji angani | | |
| 6. | Redio za VHF za mkononi | Haihusiki | |
| | | | |

Chaneli mahususi zimehifadhiwa ili zitumike kipekee kwa ajili ya kuwasiliana na wadau walioteuliwa iwapo kutatokea maafa. Masafa ya sasa ya chaneli yaliyoratibiwa katika kituo cha msingi cha redio ya HF katika Mawasiliano ya EOCC ni kama ifuatavyo;

| Taasisi | Masafa ya HF | Namba ya Chaneli: Jina | Maelezo ya chaneli |
|---|---|---|---|
| EOCC | | | |
| Msalaba Mwekundu | | | |
| Afya | | | |
| TMA | | | |
| Gari la wagonjwa | | | |
| Polisi | | | |
| Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | | | |
| TPDF | | | |
| GST | | | |
| TASAC | | | |
| TCAA | | | |
| TAA | | | |
| TANESCO | | | |

Masafa ya chaneli ya VHF yaliyopangwa katika redio ya VHF kwenye chumba cha Mawasiliano cha EOCC na magari ni kama ifuatavyo;

| Chaneli ya VHF | Kusambaza masafa (Tx (MHz)) | (Kupokea msafa (Rx (MHz)) | Maelezo ya chaneli |
|---|---|---|---|
| EOCC | | | |
| | | | |
| | | | |
| Kongani ya Utendajikazi/Uendeshaji | | | Polisi, Moto, Gari la Wagonjwa, |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

### 3.2 Ratiba ya Majaribio:

Kila mwezi, Ofisa Mawasiliano atapaswa kufanya ukaguzi wa redio na vituo vyote vya mtandao wake (VHF na HF). Jaribio hili litasaidia kutuhakikishia kuwa, mfumo unafanya kazi kama ilivyotarajiwa.

Ratiba ya majaribio ya ukaguzi wa redio itaandaliwa na Ofisa Mawasiliano na wahusika wengine wote (mf. TMA, Polisi, Zimamoto) atakaowasiliana nao katika ukaguzi wa kila mwezi wa redio, watapaswa kuelewa kuwa, watatarajia Mawasiliano kwa njia ya simu ya upepo. Kutotoa ushirikiano kwenye ukaguzi wa redio kutawekwa kwenye kumbukumbu na Ofisa Mawasiliano na kisha kuwasilishwa katika ripoti ya wiki itakayotolewa na Ofisa Mawasiliano kwenda kwenye menejimenti.

Kama sehemu ya majaribio ya kila mwezi ya redio, ukaguzi wa msingi wa redio za EOCC utafanywa na Ofisa Mawasiliano ili kuhakikisha kuwa, vifaa vimechajiwa kikamilifu, antena zimefungwa vizuri na vifaa viko tayari kwa matumizi ya papohapo.

## 4.0 MAWASILIANO YA SATELAITI

### 4.1 Simu za Satelaiti

EOCC ina simu za setelaiti na vituo vya Mtandao wa Eneo la Kimataifa la Bendi Kubwa (BGAN) kwa ajili ya uunganishaji wa data. Kitabu cha simu kilichohuishwa kitakuwa na anwani zote muhimu zenye simu zao za satelaiti na namba za simu za setilaiti.

### 4.2 Kituo Kidogo Sana Kinachopitisha Mawimbi ya Data, Sauti na Video za Satelaiti (VSAT)

EOCC kina vifaa vya ..... VSAT tuli na ........... chepesi ambacho kinaweza kusambazwa kwenye dharura.

## 5.0 MFUMO WA USAFIRI WA ANGA USIOKUWA NA RUBANI (DRONES)

EOCC wana.... Ndege zisizo na rubani (drones) ..................... Ndege zisizo na rubani za Zimamoto na za Utafutaji na Uokoaji

## KIAMBATISHO II: MAOFISA WENYE WAJIBU WA KUTOA HUDUMA ZA MAWASILIANO KATIKA VITUO VYA KUDHIBITI MAAFA

### A. Taarifa za Mawasiliano ya Kituo cha Taifa cha Mawasiliano ya Utendajikazi wa Dharura

| Na. | Jina na Uteuzi | Jina Mbadala na Uteuzi | Taasisi/Kampuni | Taarifa za Mawasiliano [Simu ya Mkononi na Baruapepe] |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

EOCC kitapaswa kufanya kazi saa 24/7

### B. Taarifa za Mawasiliano ya Viongozi/Watu wa Kuwasiliana nao Kitaifa (Mkoa, Wilaya)

| Na. | Jina na Uteuzi | Jina Mbadala na Uteuzi | Taasisi/Kampuni | Taarifa za Mawasiliano [Simu ya Mkononi na Baruapepe] |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

### C. Taarifa za Mawasiliano ya Watoa Huduma za Mawasiliano wanaohusika na dharura na maafa

| Na. | Jina na Uteuzi | Jina Mbadala na Uteuzi | Taasisi/Kampuni | Taarifa za Mawasiliano [Simu ya Mkononi na Baruapepe] |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

## KIAMBATISHO III: TAARIFA KUHUSIANA NA KUTOKEA KWA MAAFA

Itatumwa kwenda TCRA na watoa huduma, ndani ya muda usiozidi saa 24 baada ya kutokea kwa maafa: (dg@tcra.go.tz).

Tarehe ya Ripoti:

Jina la Mtoa Huduma:

A. Aina ya Maafa:
B. Tarehe na Wakati wa Kutokea:
C. Eneo Lililoathirika (Idadi na Majina ya wilaya zilizoathirika):
D. Tathmini ya Vihatarishi Awali:

| Na. | Kipengee | Athari Zilizopo | Athari Zijazo | Hali mbaya zaidi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya watumiaji wakuu wa huduma walioathirika | | | |
| 2. | Idadi ya watumiaji walioathirika | | | |
| 3. | Idadi ya mabadiliko yaliyoathiriwa | | | |
| 4. | Idadi ya Minara/Vifaa vya Kusambaza na Kupokea Mawasiliano (BTS) iliyoathirika | | | |
| 5. | Idadi ya viungo vya OFC/MW/satelaiti vilivyoathirika | | | |
| 6. | Swichi zozote kuu zilizoathiriwa | | | |
| 7. | Huduma zilizoathirika | | | |

E. Hatua itachukuliwa kwa ajili ya urejeshaji wa hali ya awali, mifumo rudufu ya Mawasiliano na uanzishaji/ufunguaji wa simu za msaada wa maelezo mafupi:
F. Msaada wa haraka wa rasilimali utahitajika:
G. Taarifa nyingine yoyote muhimu
H. Wakati/tarehe ya kuhuisha taarifa inayofuata:

Jina: Mawasiliano:

Saini: Muda wa Kutolewa kwa Ripoti: